Hijjah Mabrur na Umrah

Hijjah Yenye Kukubaliwa Na Kutekelezwa

Katika Mazingira Ya Kiroho

Othman Nuuri Topbash

Dar es Saalam 2014

As-Salaam Islamic Center

Plot 354 Mbezi Beach, Makonde, Dar Es Salaam - Tanzania

Cell: +255 254 734 362,

Email: aic2013@gmail.com

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kutolesha sehemu yoyote ya toleo hili, kuitunza katika mfumo utakaowezesha kunakiliwa au kukisambaza katika aina au namna yoyote ile, iwe elektroniki, kuchapa, kunakilisha, kurekodi au vinginevyo bila kupata ruhusa kutoka kwa mwenye haki miliki.

ISBN: 978-9944-83-690-6

Mwandishi:	Othman Nuri Topbash
Msimamizi Mkuu:	Abdi Mohamed Adam
Mfasiri:	Aziza A. Ngume
Mhariri:	Ibrahimu H. Kabuga
Msanifu jalada:	Altinoluk Graphics
Kupangiliwa vizuri na:	Sarkhan Isgandarov
	Nijat Garibov

Hijjah Mabrur na Umrah

HIJJAH YENYE KUKUBALIWA NA KUTEKELEZWA
KATIKA MAZINGIRA YA KIROHO

Othman Nuri TOPBASH

YALIYOMO

DIBAJI 7

HIJJAH MABRUR NA UMRAH 17

Mlima Arafat 31

Muzdalifa Na Kuchinja 34

Mina Na Kumpiga Mawe Shetani 40

Kukimbia Baina Ya Vilima Vya Safa Na Marwa (Sa'i) 44

Ka'bah Tukufu 45

Kabla Kifo Hakijabisha Hodi 49

Kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu Na Kujisalimisha Kwake 52

Muongozo Wa Kiroho Kwa Ajili Ya Hijja Na Umrah Yenye Kukubaliwa 58

KUZURU MADINA 87

DIBAJI

Himidi za milele zinamstahiki Mwenyezi Mungu Mtukufu, aliyetujaalia baraka ya imani na kutufungulia njia nyingi za kukutana Naye kupitia matendo mbalimbali ya ibada!

Amani na Baraka za milele zimfikie Mtume Muhammad, kiigizo bora cha kuigwa na wanadamu, nuru ya uwepo wetu, kiongozi wetu, na mwombezi wetu siku ya kiyama!

Wanadamu wana mahitaji mengi. Baadhi yake ni mahitaji ya lazima kulinda uhai na maisha ya binadamu. Kwa mfano maji, hewa na chakula ni muhimu sana kwa mwili. Hali kadhalika kuna mahitaji ya kiroho ambayo ni muhimu pia, na mahitaji yake yanaweza kuwa muhimu zaidi kuliko yale ya mwili; kwa maana mwisho wa mwili ni kuingia ardhini na kuoza, wakati roho hudumu milele.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anaelezea riziki ya kimaanawi kwa mwanadamu katika Qur'an kama ifuatavyo:

"Na katika mbingu ziko riziki zenu na mliyoa-

hidiwa." (Al-dhaariyat 51: 22)

Kisha aliwajaalia waja wake matendo mbalimbali ya ibada kama njia ya kuweza kufika kwake. Ndio maana, japokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ameamrisha matendo mbalimbali ya ibada, binadamu ndio wenye kuyahitajia zaidi, kwa sababu matendo haya ni ya muhimu kwa ustawi wa kimaanawi na wa kiroho wa mwanadamu. Ustawi huo hauwezi kupatikana katika chanzo kingine chochote. Katika dunia ya leo wasioutambua ukweli huu hawana la kufanya zaidi ya kuzishuhudia roho zao zikifadhaika sana; ilihali wale wanaobahatika kuzistawisha kikamilifu roho zao huishi maisha mengine kabisa ya amani na na utulivu. Waumini huyabadilisha matatizo na huzuni za ulimwengu huu kuwa raha na furaha, na hivyo kuendelea kuishi kwenye njia iliyonyooka. Maisha yao hufyonzwa na upendo wa Mwenyezi Mungu na upendo na burudiko hili la kimaanawi na kiroho huwalinda wasitumbukie katika hatari za dunia hii.

Kwamaneno mengine, matendo fulani ya ibada yameletwa ili kukidhi mahitaji ya kiroho ya mwanadamu na kumlinda asigeuke kuwa mja mtovu wa shukrani za neema na Baraka zisizokwisha za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Matendo hayo ya ibada ni mfano wa maelekezo yanayondikwa na daktari kuwapa wagonjwa wake. Mara

nyingi watu hawatekelezi kikamilifu ibada zao kwa sababu ya uvivu au kwa kutojua siri za jambo hilo. Ndio maana Mwenyezi Mungu Mtukufu ametaka kuwalinda waja wake wasinyimwe manufaa na faida za matendo mbalimbali ya ibada na hivyo akayafanya baadhi yake kuwa wajibu na faradhi kwa waumini.

Hakika **ibada ya swala** inaongoza ibada hizi muhimu. Hii ni kwa sababu ndiyo iliyokuwa ibada ya kwanza kufaradhiswa. Kwa kweli, swala zinazotekelezwa kikamilifu zinaweza kuondosha vifuniko vilivyoufunika moyo wa mwanadamu na kupata muungano wa ajabu na Mola wake kama ishara maneno yasemayo **"swala ni miiraj ya muumini."** Muungano huu hujidhihirisha kwa muumini baada ya yeye kuitii amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo **"Sujudu na ujongee!"**[1] (Alaq 96: 19).

Baada ya ibada ya swala, inafuatia **funga** kama ibada ya faradhi inayozistawisha roho zetu. Funga ni ibada kubwa inayokuza maadili ya mtu kwa kuimarisha subira, utashi, na kupambana na mata-manio ya nafsi. Huwakumbusha watu thamani ya neema mbalimbali za Mwenyezi Mungu na

1. Kwa tafsiri ya aya mbalimbali za Qur'an kwa lugha ya Kiswahili limetumia: Tarjuma ya Qur'ani Tukufu Kwa Kiswahili ya Sheikh Ali Muhsin Al-Barwani

hutufanya tutafakari juu ya mateso mtu mwenye njaa na maskini. Funga huwafanya matajiri kuwa sawa na masikini kwa kuwafanya wapate shida na tabu inayowapata maskini, na kwa kufanya hivyo matajiri huwa na hisia ya huruma na kuwasaidia wengine.

"Zaka na Sadaka" ni mojawapo ya ibada za faradhi zinazoleta upendo na huruma, na hivyo kuondosha uaduia na chuki kati ya matajiri na masikini katika mfumo wa jamii ya Kiislamu.

Katika ibada hii kuna faida mbalimbali zisizoonekana kwa macho, kama vile kuzuia uwezekano wa mtu kuzinyenyekea mali zake na kuzuia kuibuka kwa chuki dhidi ya matajiri. Kwa namna hiyo, mizania na uwiano wa kijamii hupata kulindwa.

Mbali na ibada hizo, kuna ibada nyingine ambayo hufanyika kwa kuhusisha mwili na mali. Ibada hii muhimu inaitwa Hajj au hijja kubwa. Ibada hii huikamilisha imani kwa kutengeneza mfano wa mazingira ya siku ya hukumu hapa hapa duniani. Pia ni njia muhimu ya kumfanya mtu aelewe maana ya **"kufa kabla kifo hakijakujia."**

Vipengele vya ndani vya ibada hii ya Hijjah ni muhimu zaidi kuliko kipengele chake cha nje. Hijjah ambayo imeelezewa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) kama *Hajj Mabrur,* yaani

hijja yenye kukubaliwa, ni ibada iliyojaa jamala za kimaanawi kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Kwa mtazamo huu, hijjah ina maana ya maombi, toba, na pia kurehemewa, Baraka na neema za Mwenyezi Mungu. Hijja ni kuyabadilisha maisha haya kwa matendo mema na hutumika kutoa ahadi kwa Mwenyezi Mungu ya kudumisha mazuri yanayopatikana wakati wa hijja pindi unaporudi nyumbani kutoka kwenye maeneo haya matakatifu.

Alipokuwa akielezea matukio ya matendo mema yanayofanywa wakati wa hijja ndogo au kubwa, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alieleza faida za ibada hii kama ifuatavyo:

"Unganisha Hijja na Umra, kwa maana zinafuta dhambi kama ambavyo viriba hufuta kutu kwenye chuma." (Nasai, Manasik, 6; Ibn Majah, Manasik, 3)

Umrah, au hijjah ndogo, ambayo imeshauriwa katika hadith hii kuchanganywa na hijja kama njia ya utakaso, nayo pia ni ibada muhimu katika Uislamu.

Tofauti na Hijjah ambayo hutakiwa kutekelezwa mara moja tu na katika masiku kadhaa ya mwaka, Umrah inaweza kufanyika kipindi chochote ndani ya mwaka na mara nyingi kwa jinsi mtu awezavyo. Vilevile umra huitwa "hijja ndogo" kwa sababu ya thawabu na fadhila nyingine zin-

azopatikana ndani yake. Ni vyema pia mtu akajua ubora na faida zake.

Kitu cha kukumbukwa zaidi katika ibada zote hizi ni lile sharti la kwamba zinatakiwa kutekelezwa kwa ikhlas na kwa moyo safi. Kama tunahitaji utiifu wetu ukubalike mbele za Mwenyezi Mungu Mtukufu, juhudi zetu zote zinapaswa kuelekezwa kwenye kuzitelekeza ibada zetu kwa moyo wa upendo na ndani ya mipaka ya tabia njema. Hapo ndipo matendo yetu yatakapopata sifa ya kuwa matendo mema na kuwa chakula cha furaha katika ulimwengu wa milele baada ya kufa.

Katika kazi hii ndogo, nimejaribu kuelezea upande wa kiroho wa Hijja na Umrah na adabu muhimu kwa ajili ya kuzitekeleza ndani ya mipaka ya uchamungu. Katika muktadha huu, nimerejea na kuchagua katika maandishi yangu yaliyokwisha chapishwa katika vitabu na makala; hivyo nimeandaa kijitabu hiki kwa ajili ya wale wanaotafuta taarifa kwa mukhtasari na zilizopangiliwa vizuri kuhusu upande wa kiroho wa ibada ya hijja katika Uislamu.

Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atujaalie uwezo wa kutekeleza ibada zote kwa ikhlas na uchamungu! Ajalie ibada zetu za swala kuwa maswahiba zetu wa milele, zaka na sadaka ziwe chakula chetu, funga na hija ziwe marafi-

ki zetu kwenye njia ielekeayo Akhera! zidumu, sadaka na zaka kuwa riziki, funga na hijjah kuwa rafiki zetu katika njia ya kuelekea akhera! Mola wetu tujaalie tuwe wenye kufanikiwa kutekeleza wajibu wetu katika njia iliyo bora!

Amiin!

Othman Nuuri Tobash
Agosti 2006
Üsküdar, İstanbul

HIJJAH MABRUR NA UMRAH

Kama moja kati ya nguzo tano za uislamu, Hijjah ni ibada inayohusisha mwili na mali. Utekelezaji wa ibada hii bora hutegemea hali ya juu ya moyo na ukamilifu wa imani nahali ya kiroho.

Hijjah ni ibada tukufu iliyoanza tangu enzi za Adam (a.s), ambaye ni kiunzi cha kwanza katika nyororo ya mitume, na kuendelea mpaka kwa Mtume wa mwisho Mtume Muhammad (s.a.w). Hijja ni njia na zana ya kuelewa maana halisi ya "kufa kabla kifo hakijakufikia."

Familia ya wanadamu kuanzia kwa Adamu na Hawa walilifanya eneo ilipo Ka'bah katika mji wa Makkah kuwa sehemu yao ya kwanza ya kufanyia ibada ili kuishi katika hali ya amani na furaha ya kidini. Kutokana na hali ya mabadiliko ya watu na jamii wana wa Adamu walitawanyika duniani kote. Karne zilipita; vizazi na vizazi vikapita, na watu wakapotoka kutoka katika njia iliyonyooka. Kwa masikitiko, eneo hili tukufu la ibada lilipotea. Kwa amri ya Mwenyezi Mungu mtukufu, Nabii Ibrahim (a.s) akaijenga upya na kupata baraka za maombi yake. Hili limeelezewa ndani ya Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

“Na Ibrahim alipo sema: Ewe Mola wan gu Mlezi! Ujaalie mji huu uwe wa amani, na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu. Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika hayo yamewapoteza watu wengi. Basi aliye nifuata mimi huyo ni wangu, na aliye niasi, hakika Wewe ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu. Mola wetu Mlezi! Hakika mimi nimewaweka baadhi ya dhuriya zangu katika bonde lisilo kuwa na mimea, kwenye Nyumba yako Takatifu, ewe Mola wetu Mlezi, ili washike Sala. Basi zijaa-lie nyoyo za watu zielekee kwao, na waruzuku matunda, ili wapate kushukuru.” (Ibrahim 14; 35-37)

Hijja ilikuwa ikifanyika katika zama za kabla ya Uislamu; lakini waabudu masanamu waliib-adili sifa yake na kuwa ni sherehe iliyojaa utovu wa maadili na kufanywa kwa ajili ya wale wenye mamlaka. Watu wa makabila ya Kiarabu walikuwa wakiizunguka Ka’bah wakiwa uchi isipokuwa Maquraish waliokuwa na hadhi ya juu. Maquray-shi walikuwa na ukarimu wa kuhakikisha wenzao wanasitiri sehemu zao za siri. Kwa maneno men-gine Maquraish waliwapa nguo ili wapate kuvaa, vinginevyo wangeizunguka Ka’bah wakiwa uchi. Wakichinja mnyama walikuwa wakipaka damu yake kwenye milango na kuta za Ka’bah na kucho-ma nyama yake.

Hatimaye, alipokuja Mtume Muhammad

Mustafa (s.a.w) na kuibuka kwa zama za furaha, maisha ya dini yalifikia kilele chake mahali pale pale yalipoanzia. Uislamu ulivunja kabisa tamaduni na imani potofu zote hizo za aibu; kwa maana ya ibada katika uislamu ni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kumuomba msamaha.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) aliishi na kuwawezesha watu kuishi katika zama za furaha zilizoizunguka Madina na Makkah. Ndio maana miji hii ikawa miji mitakatifu, mahali ambapo mapigo ya moyo wa Uislamu na Waislamu utaendelea kupiga mpaka mwisho wa dunia.

Maeneo haya matakatifu ya hijja yamemwagiliwa kwa machozi ya waumini na kustawishwa kwa hali ya kiroho ya waumini tangu Adam (a.s). Wale wanaoitekeleza ibada ya Hijjah kwa moyo wa utambuzi huyashuhudia haya na alama nyingine za kimaanawi za mitume wengi. Huhamasishwa na kuvutiwa na kumbukumbu zao; kwa sababu, maeneo haya yenye msisimko na yenye utukufu yamejaa kumbukumbu za mitume. Daima, rehma, neema na baraka za Mwenyezi Mungu hukumbukwa na watu wakiwa mahali hapa.

Lengo jingine la Hijjah ni kuziheshimu ishara za Mola wetu zinazopatikana katika maeneo haya Matukufu na kuziamsha roho zetu kwa kuzitafakari kumbukumbu hizi tukufu.

Wale wenye kuyatembelea maeneo haya kwa lengo la kufanya Hijjah au Umrah huingia na kupata heshima ya baraka za dua ifuatayo ya Nabii Ibrahimu (a.s):

"Ewe Mola mlezi wetu! Tujaalie tuwe ni wenye kusilimu kwako, na pia miongoni mwa vizazi vyetu wawe umma uliosilimu kwako. Na utuonyeshe njia za ibada yetu…" (Al-Baqara 2; 128)

Haya na bara na ishara nyingine nyingi huzichochea nyoyo za waumini kwa shauku na hamu kutembelea maeneo haya matukufu. Misafara mingi ya wampendao Mwenyezi Mungu hupaza sauti huku wakisema maneno yafuatayo:

"Nimekuwa kipofu wa mbali na karibu

Ewe Ka'bah nzuri! Natamani kuja kwako"

Au kwa mistari ya

"Ewe upepo mwanana! Kama utapita sehemu hizo mbili takatifu

Fikisha salamu zangu kwa Mtume wa watu na majinni."

Na hivyo, hutuma salamu zao na kila la kheri kwenye sehemu hizi na kwa bwana wa walimwengu kwa kusema *"Ee upepo wa asubuhi! Kama utafanikiwa kupita Makkah na Madina, fikisha salamu zangu kwa Muhammad (s.a.w) Mjumbe wa watu na majini."*

Shauku na upendo huu umeota mizizi ndani ya nyoyo za waumini kiasi kwamba imekuwa desturi kuwatuma wale wote wanaokwenda Hijjah dua na salamu. Mshairi mmoja anaakisi salamu za upendo zinazopenyezwa katika masikio ya mahujaji kama ifuatavyo:

Katika njia mpitayo
Pelekeni salamu zetu.
Kwa waumini wanaosema kuwa
Mwenyezi Mungu ni rafiki yetu
Wapelekeeni salamu zetu.

Nendeni mkatekeleze hijjah yenu
Mfikie furaha isiyo na mwisho
Kwa Muhammad Mustafa
Pelekeni salamu zetu.

Makkah na Madina
Ni hazina za kipekee
Kwa mpendwa adhimu
Pelekeni salamu zetu.

Endeleeni kusema labbaik
Yakimbilie maji ya zamzam
Kwa kizazi cha Hashim
Pelekeni salamu zetu.

Vaeni ihram
Bila kuguswa na haramu
Kwa maswahaba waliobarikiwa
Pelekeni salamu zetu.

Mtuombee kwa Mola wetu
Mtuombee dua
Kwa Ka'bah yetu tukufu
Pelekeni salamu zetu.

Wale wote wanaoingia katika bustani ya upendo
Hawataanguka kwenye mtego wa kughafilika
Kwa mlima mzuri wa Nuru
Pelekeni salamu zetu.

Ingieni ndani ya moyo wa Hatim
Msujudieni Mwingi wa Rehma
Kwenye kisimamo cha Ibrahim
Pelekeni salamu zetu.

Kwenye adhama ya Mola wetu
Kwenye mbawa zote zilizotandazwa
Kwenye Mina, kwenye Arafa
Pelekeni salamu zetu.

Kwenye bustani ya Baqi
Kwenye busani yetu safi ya mawaridi.
Kwenye furaha yetu
Pelekeni salamu zetu.

Katika historia, wale wanaompenda Mwenyezi Mungu ambao hawakuweza kuzipoza shauku za nyoyo zao waliyakata masafa kimiujiza na kuyakimbilia maeneo haya matukufu kwenda kufanya ibada zao. Baadhi yao waliweza hata kwenda pamoja na masikini wanaompenda Mwenyezi Mungu ambao hawakuwa na nyenzo za kusafiria. Kisa kifuatacho kuhusu Aziz Mahmud Hudayi ni kisa maarufu sana kuhusu jambo hili:

Alipokuwa jaji wa Bursa kesi ya ajabu ililetwa kwake. Mwanamke mmoja alikuwa akilalamika kuhusu mumewe akisema:

"Mheshimiwa hakimu! Kila mwaka mume wangu anapanga kwenda kuhiji, lakini kutokana na umasikini tulionao hakuwahi kupata bahati ya kutimiza malengo yake. Mwaka huu alisisitiza kuwa ataenda Hijjah. Alifikia hatua ya kusema kuwa:

"Kama sikwenda Hijjah mwaka huu nitakupa talaka." Kisha karibu na siku za kuchinja akaondoka. Baada ya siku tano au sita hivi alirudi na kusema kuwa amekwenda Hijjah. Je hili linawezekana vipi? Mheshimiwa hakimu! Nataka muongo huyu anipe talaka yangu."

Jaji Mahmud alimuita mume wa mwanamke yule kujua usahihi wa madai yale. Alimuuliza kama yaliyosemwa na mkewe ni kweli au la. Yule bwana akajibu:

"Mheshimiwa hakimu! Ni kweli, tunachozungumza mie na mke wangu ni kweli. Tambua kuwa ni kweli nilienda Hijjah. Huko nilikutana na baadhi ya mahujaji kutoka Bursa na niliwapa zawadi wapeleke Bursa." Akishangazwa na majibu haya Jaji Mahmud akauliza tena:

"Inawezekana vipi hili kuwa kweli?" Yule bwana akaanza kusimulia:

"Kama ilivyokuwa kwa miaka ya nyuma, nilipokuwa sina uwezo wa kwenda Hijja, nilimwendea Eskici Mehmet Dede kwa huzuni kubwa. Alinitaka nishike mikono yake na kisha nifumbe macho. Nilipofumbua macho nilijikuta niko kwenye Ka'bah." Kwa kuwa hakuwahi kushuhudia tukio kama hilo hapo kabla, Jaji Mahmud hakukubaliana na maelezo hayo. Hapo yule bwana masikini, ambaye bado alikuwa ameathiriwa na hali ya kiroho ya maeneo hayo matakatifu, alitoa jibu lenye kuchemsha akili:

"Mheshimiwa hakimu! Kama ibilisi ambaye ni adui mkubwa wa Mwenyezi Mungu ana uwezo wa kusafiri duniani kote, kwanini rafiki wa Mwenyezi Mungu asiweze kwenda kwenye Ka'bah kwa muda mfupi?"

Jaji aliona kuwa jibu lile ni zito sana, akaahirisha kesi hadi mahujaji watakapokuwa wamerudi kutoka hijja. Pindi mahujaji wa Bursa waliporudi,

alithibitisha kuwa ni kweli bwana huyu alikwenda kuhijj. Kwa hiyo alilazimika kuifuta kesi hiyo. Lakini, hakujisikia raha, kwa hiyo akakutana na mwalimu wake Uftada (q.s) kupitia kwa Eskici Dede Efendi na kuwa mmoja kati ya masultani wa nyoyo.

Yatupasa tukumbuke kuwa shauku na upendo wa kuyapenda maeneo haya matukufu havipatikani kwa kuona tu muonekano wake wa nje au majangwa yake ya mchanga. Hupatikana kwa kuitembelea maqaam Ibrahim (a.s) na makazi ya mwanae Ismail (a.s). Hupatikana kwa kuiona ardhi aliyozaliwa Mtume Muhammad (s.a.w), alipokulia na alipoufikishaa ujumbe wa Uislamu.

Lengo jingine la hijjah ni kuvuta hewa na kuiweka nyoyoni mwetu taswira ya ardhi aliyoishi Mjumbe huyu mtukufu wa Mwenyezi Mungu. Mshairi analielezea hili kwa uzuri kabisa:

"Kila ninapogeuza macho yangu, miujiza isiyohesabika huunyakua moyo wangu na kusema: "hili ndilo eneo halisi."

Haya si maneno ya ushairi tu lakini yenye uhalisia wa ajabu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anaeleza ndani ya Qur'an Tukufu:

فِيهِ اٰيَاتٌ بَيِّنَاتٌ

"Ndani yake zipo ishara zilizo wazi…" (Al-i Imran 3: 97)

Kwa hiyo katika ardhi hizi takatifu, wale watakaoondosha vizuizi vya mghafala ndani ya nyoyo zao na kutazama kupitia dirisha la roho zao wataziimarisha imani zao na upendo wa Mwenyezi Mungu utayazunguka maisha yao yote. Wana-pogeuza nyuso zao, hali ya furaha na shauku ya kimaanawi huwaenea. Macho yao huanza kububujikwa machozi na ndimi zao zikishughulika kumsifu na kumhimidi Mwenyezi Mungu bila kuchoka na kuutangaza Umoja Wake. Hutumia muda wao mwingi katika hali ya utiifu na maadili ya hali ya juu. Na hii ni baraka kubwa kutoka katika siri ya aya ifuatayo:

ذٰلِكَ وَمَنْ يُعَظِّمْ شَعَائِرَ اللّٰهِ فَاِنَّهَا مِنْ تَقْوَى الْقُلُوبِ

"Ndivyo hivyo, na anayetukuza ibada za Mwenyezi Mungu, basi hayo ni katika unyenyekevu wa nyonyo." (Al-Hajj 22:32)

Kwa hiyo hijja siyo ibada ya kimwili na ya dhahiri tu. Bali pia ina upande wa ndani ambao ni muhimu zaidi kuliko muonekano wa nje. Hijja ambayo iliitwa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu

(s.a.w) kama *Hajj mabruur*, yaani hijja yenye kukubaliwa, ni ile inayoundwa na uzuri wa ndani kuanzia mwanzo mpaka mwisho.

Kwa muktadha huu basi, Hijja ni maombi, toba, na kupata rehma, baraka na fadhila za Mwenyezi Mungu. Huyaboresha maisha haya kwa matendo mema. Pia tunapokuwa katika ibada hii hutoa ahadi kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa tutakaporudi nyumbani tutahakikisha tutayalinda yale yote tuliyopata kipindi cha hijja.

Uzuri ulioje wa dua Nabii Ibrahim (a.s) pindi alipoomba akisema:

"Ewe Mola mlezi wetu! Tujaalie tuwe ni wenye kusilimu kwako, na pia miongoni mwa vizazi vyetu wawe umma uliosilimu kwako. Na utuonyeshe njia za ibada yetu na utusamehe. Bila shaka wewe ndiye mwenye kusamehe mwenye kurehemu." (Al-Baqara 2:128)

Nyoyo zenye mapenzi ambazo hupata bahati ya kuhiji huimarika kwa dua mbalimbali huku zikitafakari kuwa ziko ndani ya mipaka ya ardhi takatifu ambayo Mtukufu Mtume (s.a.w) aliishi. Huhisi msisimko anapowaza kuwa yumkini akawa anakanyaga sehemu iliyokanyagwa na Mtukufu Mtume (s.a.w). Wanapotembelea vilima vya Safa, hufikiria, kwa mfano, kuhusu hotuba ya Mtukufu Mtume (s.a.w) alipowahutubia Maquraish

waabudu masanamu. Hukumbuka kwamba katika mlimahuo ndipo Mtukufu Mtume (s.a.w) alipowaambia Maqurayshi, akiwaonyesha mlima wa Abu Qubays:

"Nikiwambieni kuwa kuna farasi upande wa pili wa mlima huu wanaotaka kuwavamia mtaniamini?" Watu wa Makkah wakajibu:

"Ndio, hata kama hatukioni kilicho nyuma ya mlima, hatuna shaka yoyote kwa utakachotwambia kwa maana wewe ni Muhammad al-Amin (Muhammad muaminifu)." Baada ya kusikia jibu hilo, Mtukufu Mtume (s.a.w) akasema:

"Kama mnavyoniamini, basi aminini kuwa kuna Mwenyezi Mungu aliyeumba huu ulimwengu, na ambaye ni Mungu mmoja na Mwenye Nguvu. Masanamu mnayoyaabudu si chochote bali ni vipande vya mawe na mbao tu. Viacheni na mumuamini Mungu mmoja. Tambueni kuwa Mwenyezi Mungu amenileta kama Mtume kwenu." Makafiri, akiwemo ami wa Mtume (s.a.w), Abu Lahab wakamwambia:

"Umetukusanya hapa kwa hili tu au kuna jingine?" Wakaondoka na kumuacha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w). Japokuwa waliutambua na kuukubali uaminifu wake, waliukataa ujumbe wake kwa sababu ya ubinafsi.

Pamoja na yote hayo, alikuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa walimwengu, hivyo hakukata tamaa mbele ya mghafala kama huo wa kutomsikiliza. Aliendelea kufikisha ukweli wa Mwenyezi Mungu kwa nyoyo zenye kiu wakati wote na katika mazingira ya aina yoyote ile.

Tunapozitafakari nyakati hizo na kujitazama tukiwa katika hali hiyo ya kiroho, tunaweza kuhisi kana kwamba tunashuhudia tukio adhimu lililotokea katika nyumba ya Arqam. Mara tukio la Hijra (tukio la kuhama kutoka Makka kwenda Madina) hupenya ndani mwetu, na kutaamali baraka zilizoambatana na tukio hilo.

Yumkini tunaweza kuwa sehemu ya mawasiliano ya kiroho na kimaanawi uliotokea baina ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) na sahibu wake, Abu Bakr (r.a), katika pango la Thawr na manufaa yatokanayo na siri yake kwa kadiri ya kiwango tutakachoweza kulielewa kiundani tukio hili. Baada ya hapo nyoyo zetu zinaweza kupata utamu wa imani iliyotokana na furaha ya nyororo ya dhahabu iliyoanzia kwenye mazungumzo baina ya wawili hao.

Baada ya kuonja ladha ya imani, tunaweza kuwafuata maswahaba wa Mtume (s.a.w), walioishi kama nyota, na kutafakari jinsi gani waliishi Madina na kisha wakaikomboa Makkah chini ya

uongozi wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w).

Tukiitazama milima ya Makkah, huvuta taswira ya maelfu ya moto yaliwashwa na maswahaba kuwatisha na kuwatia khofu watu wa Makkah. Huvuta taswira ya sauti ya adhana ikitolewa na Bilal Habashi (r.a) siku hiyo juu ya paa la Ka'bah. Vilevile tunaweza kuvuta picha ya jinsi Mtume wetu (s.a.w) alivyoyavunja masanamu yaliyokuwa ndani ya Ka'bah huku akisoma aya ifuatayo:

"…Kweli imefika, na uwongo umetoweka…"
(Al-Isra 17: 81)

Tukumbuke kuwa, kama ambavyo Kaabah iliwahi kujazwa masanamu, nyoyo zetu pia zinaweza kujazwa masanamu ya matamanio yetu. Tunaweza kuyavunja masanamu haya kwa nguvu za kiroho tunazozipata katika kila hatua ya hijja yetu na kuzibadilisha nyoyo zetu kwa mahala panapotazamwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Hijja, ambayo ni mlango wa kupata ishara na utambuzi kama huu, ni tukio la utakaso, utulivu na ufufuo wa kimaanawi na kiroho. Hijja ni ibada adhimu ambayo humuongoza mtu kwenye kuikamilisha dini yake.

Hijjah ina maana ya kuuvua mwili na nafsi na kuingia katika ulimwengu wa kiroho. Ni ibada ambayo mja huweza kuipata rangi, hali na mua-

faka wake wa kiroho, na pia kupata utambulisho halisi. Katika hijjah mja hutakasika kwa maji ya nuru na utambuzi. Ni ibada iliyojaa ishara kayaya za hali ya kiroho.

MLIMA ARAFAT

Arafat ni mahali pa msamaha na kimbilio. Arafat inatukumbusha kuwa watu watafufuliwa kutoka kwenye makaburi yao ya Siku ya Mwisho na kukusanyika kwa umati kwenye sehemu ya hukumu ya mwisho. Siku hiyo, waja wa Mwenyezi Mungu watakuwa wakisubiri kwa matarajio msamaha mbele ya Mwenyezi Mungu.

Kwenye mlima huu, nyoyo na macho huvimba kwa machozi ya kuomba msamaha. Dua na maombi huelekezwa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mja huanza upya maisha yake na kumuahidi Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa ataendelea kuishi maisha yaliyobaki katika utii.

Kwa hiyo mlima Arafat unawakilisha picha ya siku ya mwisho. Baadhi ya picha za Siku ya Kiyama hupatikana hapo. Hakika hutukumbusha hali ya kufufuka kutoka makaburini, kukusanyika sehemu ya hukumu, tukiwa tumekata tamaa, na kuomba kwa dhati huruma ya Mola wetu. Ni kipindi cha kuacha vyeo vyote vya kidunia na kuingia mbele ya Mwenyezi Mungu ukiwa na vipande viwili tu vya nguo.

Kwa upande mwingine, Arafat hutupeleka kwenye kumbukumbu za kale. Kama tujuavyo, kutokana na kula tunda walilokatazwa, Adam (a.s) na Hawa walifukuzwa peponi na kupelekwa ardhini, huku kila mmoja akishushwa sehemu ya mbali na mwenzake. Hivyo kila mmoja alimkumbuka mwenzake.

Adam (a.s) aliomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa cheo cha Mtume Muhammad (s.a.w) kwa kutambua utukufu na heshima yake mbele ya Mwenyezi Mungu. Maombi yake yalisikilizwa, na Mwenyezi Mungu Mtukufu akamtuma malaika amuonyeshe Adam (a.s.) njia ya kwenda Makkah. Na kutokana na dua na maombi ya Adam (a.s), mama yetu Hawa alichukuliwa na malaika mwingine hadi kwa Adam (a.s). Walikutana kwenye bonde la Arafat alasiri ya siku husika. Wakalia na kutubu dhambi zao.

Sio tu kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyakubali maombi yao, bali pia aliwajaalia na kuwaahidi kuwa atavisamehe na vizazi vyao kila mwaka pindi watakapokuja kuomba toba katika siku ile ile na muda ule ule. Hii ndio sababu inayowafanya mahujaji kwenda Arafat kuomba msamaha katika siku ijulikanayo kama siku ya *Arafah* kabla ya ‘Eid.

Baada ya kukutana, Adam (a.s) na mama yetu Hawa walichagua Makka kuwa makazi yao kwa

amri ya Mwenyezi Mungu. Ndio maana Makkah inajulikana kama “Umm al-Qura” au mama wa ardhi zote; kwa sababu ni mahali ambapo tofauti zote za kidunia, kama vile utaifa, rangi, utajir, umaskini na muonekano wa kimwili hupoteza maana yake, na waumini huwa umma mmoja chini ya undugu wa Uislamu. Makkah ni mahali ambapo, mwajiri ni mwajiriwa, tajiri na maskini, msomi na asiye msomi, wote wanakaa sehemu moja na kuvaa mavazi ya aina moja. Watu wote husimama katika safu moja. Makka ni mahali pasipokuwa na tofauti zozote za kitabaka, ni sehemu ambayo mtu huvaa mavazi ya kaburini, ni mahaliambapo mtu hurejea kwa Mola wake, na ni mahali ambapo mtu hutetemeka kwa kuyafikiria matukio ya kutisha ya Siku ya Hukumu.

Mji huu wenye baraka ni kiota cha usalama, amani na upendo; ni mji wa mitume wanazijaza nyoyo zetu kwa baraka na rehma. Leo hii, licha ya matatizo katika ulimwengu wa Kiislamu kilele cha amani, upendo, na umoja unaoletwa na hijjah kwenye ardhi hizi tukufu ni kitu ambacho mataifa mengine yanakiota. Mataifa yanafanya kila juhudi kuwa na kiwango hiki cha umoja kupitia taasisi zao za kimataifa, lakini hawajaweza kupata mafanikio kamili. Kutokana na matamanio yao ya kidunia, migongano, uadui, mipasuko, dhulma, ukandamizaji na upepo wa ubaguzi unawagawa.

MUZDALIFA NA KUCHINJA

Muzdalifa, kituo kinachofuata baada ya mlima Arafa, ni sehemu iliyojaa ishara mbalimbali za rehma. Ni moja kati ya sehemu zinazoitwa na Qur'an kama *Mash'ar al-Haram*, yaani alama za eneo takatifu. Ni mahali pa kujifunza jinsi ya kusahau kila kitu, hata maisha ya akhera, na kuelekeza nyoyo zetu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa upendo na utii.

Baada ya kukamilisha ibada mbalimbali, sadaka ya kichinjwa cha kimaada, kinachowakilisha sadaka ya kichinjwa cha kimaanawi cha Nabii Ibrahimu (a.s), ni upepo mwanana wa rehma na hekma inayowakumbusha mahujaji hisia za Mtukufu Mtume (s.a.w). Wale wanaovuta pumzi hii hukumbuka na kurudiarudia maneno ya Nabii Ibrahim (a.s):

"Hakika mimi nimeuelekeza uso wangu sawa sawa kwa aliyeziumba mbingu na ardhi, wala mimi si miongoni mwa washirikina." (Al-An'am 6: 79)

"Sema: Hakika Sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote, Hana mshirika wake. Na hayo ndiyo niliyoamrishwa, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu." (Al-An'am 6: 162-63)

Na Ibrahim alipokuwa njian kutoka Babel kwenda Damascus, alisema:

"Hakika mimi nahama, nakwenda kwa Mola wangu Mlezi; Yeye ataniongoa. Ewe Mola wangu Mlezi! Nitunukie aliye miongoni mwa watenda mema." (al-Saffat 37:99-100)

Hiki ni ishara ya safari ya kimaanawi na kiroho kutoka ulimwengu wa ndani kwenda kwa Rafiki wa Juu Kabisa. Aya ifuatayo inaeleza kuhusu Ismail na kisa cha kutolewa sadaka:

"Basi tukambashiria mwana aliye mpole." (Al-Saffat 37: 101)

"Basi alipo fika makamo ya kwenda na kurudi pamoja naye, alimwambia: Ewe mwanangu! Hakika mimi nimeona usingizini kuwa ninakuchinja. Basi angalia wewe, waonaje? Akasema: Ewe baba yangu! Tenda unavyo amrishwa, utanikuta mimi, Inshallah, katika wanao subiri." (Al-Saffat 37:102)

"Basi wote wawili walipojisalimisha, na akamlaza juu ya kipaji. Tulimwita: Ewe Ibrahim! Umekwishaitimiliza ndoto. Hakika hivi ndivyo tunavyo walipa wanao tenda mema. Hakika haya ni majaribio yaliyo dhaahiri." (al-Saffat 37: 103-106)

"Basi tukamtolea fidia kwa dhabihu mtukufu. Na tukamwachia (sifa njema) kwa watu

walio kuja baadaye. Iwe salama kwa Ibrahim! Hivi ndivyo tunavyo walipa wanao fanya mema. Hakika yeye ni katika waja wetu walio amini."
(Al-Saffat 37: 107-111)

Baada ya Ibrahim (a.s) kumuacha mama yetu Hajar na Ismail (a.s) huko Makkah, alienda kwa mama yetu Sarah. Mara kwa mara aliwatembelea Hajar na Ismail. Siku moja alipokuwa Makkah aliona ndoto. Ndani ya ndoto hiyo aliona kuwa anachinja mwanaye Ismail (a.s) kama ilivyoamrishwa kwenye aya hapo kabla. Nabii Ibrahim (a.s) alikuwa na wasiwasi kuhusiana na ndoto hiyo kama inatoka kwa shetani au inatoka kwa Mwenyezi Mungu mtukufu. Ndoto ile iliendelea kwa muda wa siku tatu. Siku hizi zilikuwa siku za *Tawriya*, siku kabla ya sikukuu ya kuchinja, na siku ya mwanzo ya *Eid*.

Kwa mujibu wa riwaya moja, Nabii Ibrahim (a.s) aliwahi kusema kabla kuwa:

"Ikiwa Mwenyezi Mungu atanijalia mtoto, basi nitamtoa sadaka kwa Mola wangu." Hii ndiyo sababu Mwenyezi Mungu alikuwa anampima.

Nabii Ibraham (a.s) akamwambia mkewe Hajar amuogeshe Ismail na kisha ampake manu-

kato. Nabii Ibrahim (a.s) akamwambia mkewe kuwa anampeleka mwanaye kwa rafiki. Akamwambia mwanae abebe kamba na kisu na kuendelea kusema:

"Mwanangu mpendwa! Nitakutoa sadaka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu." Wakafunga safari kuelekea Arafat. Mara Ibilisi akamjia Hajar katika umbile ya kibinadamu na kusema:

"Je unajua mahali Ibrahim anapompeleka mwanao?" Akajibu:

"Ndio, anampeleka kwa rafiki yake." Ibilisi akamwambia:

"Hapana, anakwenda kumchinja" Hajar akajibu:

"Anampenda mwanae."

Ibilisi akaendelea:

"Ibrahim anakwenda kumchinja mwanao kwa sababu Mwenyezi Mungu amemuamuru kufanya hivyo".

Hajar akamwambia Ibilisi:

"Ikiwa Mwenyezi Mungu ndiye aliyemwambia afanye hivyo basi jambo zuri. Tunatii amri na maagizo Yake."

Ibilisi alipogundua kuwa hawezi kumlaghai

Hajar, alikwenda kwa Ismail (a.s) na kumwambia:

"Je unajua baba yako anapokupeleka?" Ismail (a.s) akajibu:

"Kutekeleza amri ya Mola wake" Ibilisi akamtisha kwa kumwambia:

"Kama unavyojua, anakwenda kukuchinja." Ismail akamfukuza ibilisi na kumpiga mawe huku akisema :

"Toka! Ewe uliyelaaniwa. Tunataka kutekeleza maamrisho ya Mola wetu."

Ibilisi hakuweza kumlaghai Ismail. Akahamia kwa Nabii Ibraham (a.s) na kumwambia:

"Ewe mzee! Unampeleka wapi mwanao? Ibilisi amekulaghai ndotoni. Hizo ndoto ulioteshwa na Ibilisi. Nabii Ibrahim (a.s) akamwambia:

"Wewe ni Ibilisi. kaa mbali nami. " Kisha Ibrahimu akachukua mawe ishirini na moja na kumpiga nayo ibilisi katika sehemu tatu tofauti. Na hapa ndipo lilipoanzia tukio la kumpiga mawe shetani. Unyenyekevu na utii wa Nabii Ibrahim (a.s) na familia yake umekuwa mfano kwa wafuasi wa Muhammad (s.a.w).

Wakati Ibrahim (a.s) na Ismail (a.s) walipokuwa njiani kutoka Arafat kuelekea Mina, malaika wa peponi walipata msisimko sana. Walishangaa na kuambizana:

"Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu! Nabii anakwenda kumchinja Nabii."

Nabii Ibrahim (a.s) alimwelezea mwanae Ismail (a.s) kuhusu jambo hilo:

"Ewe mwanangu! Nimeagizwa nikuchinje." Nabii Ismail (a.s) akauliza:

"Ewe baba yangu! Ni Mwenyezi Mungu ndiye aliyekuagiza kufanya hivi?" Nabii Ibrahim akajibu:

"Ndio"

Hapo Nabii Ismail (a.s) akamwambia baba yake:

"Ewe baba yangu! Fanya uliyoamrishwa; Mwenyezi Mungu akipenda utanikuta kuwa katika watu wenye kufanya subira." Alimweleza baba yake kuwa alikuwa tayari kutoa uhai wake. Wakati huo Ismail alikuwa na umri kati ya miaka saba au kumi na tatu.

Kwa mujibu wa riwaya kadhaa, katika matukio matatu Malaika Jibril alikuwa na hofu iwapo atafika kwa wakati. Moja ni pale Ibrahim (a.s) alipoweka kisu shingoni mwa Ismail (a.s). Hapo, Jibril (a.s) alikifanya kile kisu kuwa butu na kuwambia kuwa kwa sababu ya utii na unyenyekevu wao wameletewa kondoo kutoka mbinguni, ambaye atachinjwa badala ya Ismail. Hivyo kondoo huyo akachinjwa na Ismail akapona.

Kwa hiyo, lengo halisi la sadaka ya mnyama ni kukumbuka matukio haya, ili tupate kufaidika na mafunzo yanayopatikana ndani yake na kuzifanya nyoyo zetu kuwa tayari kutii na kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hili limeelezewa katika Qur'an kama ifuatavyo:

"Nyama zao hazimfikii Mwenyezi Mungu wala damu zao, lakini unamfikia uchamngu wenu... " (al-Hajj 22:37)

Vile vile kunyoa nywele baada ya kuchinja ni tukio lenye maana kihistoria. Kabla ya ujio wa Uislamu mtu alipokuwa akitaka kumuacha huru mtumwa alikuwa akimyoa kichwa chake. Hii ilikuwa kama alama ya utumwa wake. Kwa kunyoa nywele zao, mahujaji huwa wamekubali utumwa wao kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa maneno mengine, tukio hili ni namna ya kuonyesha kujisalimisha mbele ya Mwenyezi Mungu mtukufu na kutangaza kuwa sisi ni watumwa wake.

MINA NA KUMPIGA MAWE SHETANI

Mina, sehemu ambayo Ibrahim na Ismail (a.s) walimrushia mawe na kumpiga shetani, ni sehemu yenye baraka inayowatia hamasa Waislamu juu ya udharura wa kumtegemea Mwenyezi Mungu na kujisalimisha Kwake.

Kwa upande mwengine, kumpiga mawe shet-

ani kunaanza na kumpiga shetani ndani ya mtu mwenyewe. Kama ilivyoelezwa mwanzo, Shetani alijaribu walaghai Ibrahim, Ismail na Hajar. Kumpiga mawe shetani, ambayo ni moja ya shuruti za hijja, ni ukumbusho wa jinsi walivyompiga na kumfukuza shetani.

Kwa njia nyingine, kurusha jiwe kuna maana ya kulaani, kwa maana zamani kulaani kulifanywa kwa kurusha. Kwa kweli, miongoni mwa sifa za shetani ni *rajiim*, lenye maana ya aliyepigwa mawe, ni sifa inayoelezea kulaaniwa kwake.

Aidha, yafaa kukumbuka kuwa kumpiga mawe shetani ni sawa na kuzipiga mawe dhambi zako. Lengo ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) anasema kuwa:

"Kumpiga mawe shetani na kukimbia baina ya vilima vya Safa na Marwa hufanywa katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu." (Tirmidhi, Hajj, 64/902)

Maana nyingine inayopatikana katika kumpiga mawe shetani ni kuonyesha uadui dhidi yake. Kwa sababu Iblisi alitakabari na kumhakiri Adam (a.s) kwa kuwa Adam aliumbwa kutokana na udongo ilihali yeye iblisi aliumbwa kutokana na moto, hivyo Mwenyezi Mungu anamtupia kitu (mawe) kinachotokana na kitu kilekile (ardhi) alichokihakiri na kukidharau.

Hisia na utambuzi unaopatikana wakati wa kumpiga mawe Shetani vinatakiwa kuingia katika vipengele vyote vya maisha yetu. Tunatakiwa kuondosha wasiwasi na kila shaka inayotupwa na shetani nyoyoni mwetu kwa kusema:

أَعُوذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

"Ninajilinda kwa Mwenyezi Mungu dhidi ya shetani aliyelaaniwa." Tunatakiwa kumpiga mawe shetani kwa kutumia maneno haya mpaka mwisho wa uhai wetu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an Tukufu:

"Na Shet'ani akikuchochea kwa uchochezi wewe jikinge kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua." (Fussilat 41; 36)

Kumpiga mawe shetani kuna maana ya kumlaani na kuitakasa nafsi dhidi ya mghafala na wasiwasi. Pia humkumbusha muumini kuuboresha moyo uliotakasa kwa kumdhukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Aidha, wakati wa hijja, mja anatakiwa kuweka suala lifuatalo akilini mwake:

Wezi huwa hawaibi katika duka la vikorkoro wakati jirani kuna maduka ya dhahabu; kwa maana utajiri upo katika dhahabu. Hili unaweza

kulilinganisha na hali ya muumini mwema anayetekeleza kikamilifu ibada zake na mtu mwingine aliyeghafilika. Shetani ambaye amepewa idhini na Mwenyezi Mungu ya kuwashawishi watu, kwanza hujaribu kuwashawishi watu wema. Hasa hasa huwashambulia na kuwadanganya wale wanaopanga kutekeleza ibada ya hijja. Ndiyo maana uvumilivu inapaswa kuwa silaha ya kwanza ambayo hujaji anapaswa kuwa nayo. Kwa sababu hijjah ni tofauti na ibada nyingine. Kwa nje inaonekana kuwa rahisi ila ni miongoni mwa ibada ngumu sana. Ndio maana mahujaji hutamka maneno yafuatayo pindi wanapotia nia ya kwenda kuhijji: "Ewe Mwenyezi Mungu! Nijaalie hijjah yangu iwe rahisi …"

Nyoyo zinazomgeukia Mwenyezi Mungu husisitiza imani yao Kwake kwa kusema:

لَبَّيْكَ اللّٰهُمَّ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ لاَ شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ،

اِنَّ الْحَمْدَ وَالنِّعْمَةَ لَكَ وَالْمُلْكَ لاَ شَرِيكَ لَكَ

"Nimekuitika Molawangu, nimekuitika. Nimekuitika huna mshirika. Himidi, neema na ufalme vyote ni vyako. Huna mshirika."

Wanajua kuwa wapo katika ardhi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na wanaahidi kuwa kuanzia wakati huo hawatalaghaiwa na hadaa za Shetani.

Waumini hawana budi kuzitambua mbinu na hadaa za shetani. Tena muumini hana budi kustahmili shida na tabu za safari hii na kujua kuwa ni mitihani ya ulimwengu huu. Kwa namna hii hatapoteza thawabu za hijja yake.

KUKIMBIA BAINA YA VILIMA VYA SAFA NA MARWA (SA'I)

Safa na Marwa ni vilima viwili vilivyobarikiwa vilivyo karibu na kisima cha zamzam. Hivi ni vilima ambavyo Hajar (r.a) alikimbia baina yake kutafuta maji kwa ajili ya mwanae Ismail (a.s). Kwa hiyo kukimbia baina ya vilima hivi kama sehemu ya Hijja ni ishara ya kumtii Mwenyezi Mungu na kukiri udhaifu wetu mbele Yake. Ndiyo maana imeongezwa katika shuruti za hijja kwa jina la *sa'i* (yaani kukimbia na kufanya juhudi). Mwenyezi Mungu Mtukufu ameelezea umuhimu wa vilima hivi kama ifuatavyo:

اِنَّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللهِ

"Hakika vilima vya Safaa na Marwa ni katika alama za Mwenyezi Mungu…" (Al-Baqara 2: 158)

Katika aya nyingine Mwenyezi Mungu mtukufu ameeleza ni jinsi gani tunatakiwa kuwa mbele ya alama zake:

"…na anayetukuza ibada za Mwenyezi Mungu, basi hayo ni katika unyenyekevu wa nyoyo." (al-Hajj 22; 32)

KA'BAH TUKUFU

Ka'bah Tukufu ni uelekeo ambao waumini huelekeza nyuso zao wakati wa swala, ambao umeamrishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu akisema:

"Sujudu na ujongee!)" (Alaq 96; 19) Kwa waumini wote wanaielekea Ka'bah, ni mahali yalipo mapigo ya moyo wa ulimwengu wa Kiislamu. Kama ambavyo moyo ni mahali pa ishara za Kimungu ndani ya mwili wa mwanadamu, vivyo hivyo kaabah ni mahali pa ishara za Mwenyezi Mungu ndani ya ulimwengu. Kwa sababu hii basi, hijjah ni ibada inayotakiwa kufanywa kwa kutambua utukufu wa Kaabah na kwa utambuzi wa moyo.

Ka'bah, ambayo pia huitwa *Baitullah* au Nyumba ya Mwenyezi Mungu, imekuwa sehemu tukufu tangu enzi za Nabii Adamu (a.s). Katika aya zifuatazo Qur'an Tukufu imeeleza wajibu wa kuitembelea Ka'bah kwa wale wenye uwezo wa kufanya hivyo:

"Hakika Nyumba ya kwanza walio wekewa watu kwa ibada ni ile iliyoko Bakka, iliyo barikiwa na yenye uwongofu kwa walimwengu wote. Ndani yake zipo Ishara zilizo wazi - masimamio ya Ibrahim, na mwenye kuingia humo anakuwa katika amani. Na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imewajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awezae njia ya kwendea. Na atakaye kanusha basi Mwenyezi Mungu si mhitaji kwa walimwengu." (Al-i Imran 3; 96-97)

Maqam-i Ibrahim au masimamo ya Ibrahim (a.s) ipo kwenye Ka'bah. Mwenyezi Mungu Mtukufu anawataka waumini watembee mahali alipotembea rafiki yake Ibrahimu na wafanye ibada ya kuzunguka karibu na sehemu yenye unyayo wake.

Hajar al-Aswad ni jiwe jeusi lililobarikiwa, ambalo mahujaji hulibusu kama ishara ya kula kiapo cha utii kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuahidi kumtii. Kulitolea salamu wakati wa kuzunguka humaanisha kuahidi kuyaacha matamanio na tamaa zetu zote za kihayawani.

Hajar al-Aswad sehemu ya kuanzia na kumalizia mzunguko wa kuizunguka Ka'bah. Takriban kila kipande katika Ka'bah kimebadilishwa tangu ilipojengwa isipokuwa jiwe jeusi. Limepigwa busu na midomo mingi iliyobarikiwa, hata ule wa Mtume Muhammad (s.a.w). Limeguswa na

mikono mingi iliyobarikiwa. Kwa sababu hiyo, limepata nafasi na daraja kubwa katika nyoyo za waumini, licha ya kwamba zamani lilikuwa jiwe la kawaida tu.

Kwa sifa hizi na nyingine nyingi Ka'bah ni kama kivuli cha Arshi hapa duniani na chanzo cha baraka. Kwa maneno mengine, ni kioo king'aracho kinachoakisi sifa za Mwenyezi Mungu za huruma na ukarimu. Ni jua, au chemchem ya nuru imulikayo ndani ya nyoyo.

Kwa mujibu wa riwaya mbalimbali kuhusu ujenzi wa Ka'bah, baada ya Adam (a.s) na mama yetu Hawaa kufukuzwa peponi, walikutania Arafat na wakaelekea pamoja upande wa Magharibi. Hatimaye walikuja mahali ilipo Ka'bah kwa sasa. Hapo Adam(r.a) akataka kuswali ili kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwakutanisha tena. Akamwomba Mwenyezi Mungu awape nguzo ya nuru ambayo walikuwa wakiizunguka Peponi. Nguzo hiyo ikatokea mahali Kaabah iliposimama leo; hivyo Adam (a.s) akaa kuizunguka kama tendo la ibada.

Nguzo hiyo ya nuru ilitoweka kipindi cha Nabii Shith (a.s) na jiwe jeusi tu ndilo lililobaki. Ndipo Shith (a.s) akajenga jengo la mche mraba sehemu ile ile na kuliweka jiwe jeusi kwenye pembe moja. Hili ndilo jiwe lijulikanalo kama

Hajar al-Aswad leo hii.

Baada ya mafuriko, jengo hili lilikaa chini ya mchanga kwa muda mrefu. Kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, Nabii Ibrahim (a.s) akaenda mahali ilipo Ka'bah na kuishi pale pamoja na mwanae Ismail (a.s) na mkewe Hajar. Akishirikiana na mwanae walichimba mahali Kaabah ilipokuwa imejengwa. Wakakuta msingi wa jengo lililojengwa na Nabii Shith (a.s) na kuijenga tena Ka'bah Tukufu kwenye msingi ule ule. Walipomaliza kujenga, Nabii Ibrahim (a.s) alimuomba Mwenyezi Mungu mtukufu akasema:

"… Mola wangu Mlezi! Ufanye huu uwe mji wa amani, na uwaruzuku watu wake matunda, wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho…" (al-Baqara 2:126)

Kwa baraka ya dua hii ya Nabii Ibrahimu (a.s), utamu wa imani na neema zimekuwepo Makka tangu enzi hizo.

Katika historia yake yote, Ka'bah imejengwa mara kumi na moja. Mara ya kwanza ilijengwa na Malaika; mara ya pili ilijengwa na Adam (a.s); mara ya tatu ilijengwa na Shith (a.s); mara ya nne ilijengwa na Ibrahim (a.s); mara ya tano ilijengwa na watu wa Amaliqa; mara ya sita ilijengwa na watu wa ukoo wa Jurhum; mara ya saba ilijengwa na watu wa ukoo wa Qusai; mara ya nane ilijen-

gwa na Maquraish; mara ya kumi ulijengwa na Abdullah ibn Zubair, mmoja kati ya warithi wa maswahaba; mara ya kumi ilijengwa na Hajjaj ibn Yusuf ; na mara ya mwisho ilijengwa na Sultani wa Kiuthmaniya Sultan Murad IV.

Heshima maalumu waliyokuwa nayo watu kwa Ka'bah hii ilionekana katika ujenzi wa mwisho. Ifuatayo ni baadhi yake:

Wakati wa utawala wa Murad IV mafuriko yalitokea huko Makkah na pande mbili za Ka'bah zikaanguka. Ridhwan Aga, msanifu mkuu wa majengo ya ikulu, alipelekwa haraka mjini Makkah kwenda kujenga. Wakati akifanya tathmini yake ya awali, msanifu huyo mkuu, aliona kuwa haifai kutumia maneno kama vile "kuanguka au kubomoka" katika kuielezea Kaaba Tukufu na badala yake akaielezea hali ilivyo kama ifuatavyo:

"Sehemu fulani na fulani ya Kaabah ilisujudu."

Vile vile tahadhari iliwekwa kwa wanyama waliokuwa wakibeba vifaa vya ujenzi wasichafue sehemu hizo tukufu.

KABLA KIFO HAKIJABISHA HODI

Hatuna budi kukumbuka kuwa uhai ni baraka ya mara moja tu aliyopewa mwanadamu na mauti

ni hatima isiyoepukika iliyowekwa na Mwenyezi Mungu kwa viumbe Wake wenye kufa. Muda wa mauti na idadi ya pumzi vimeshapangiliwa kwa undani kabisa. Ni jambo la dhahiri kuwa kifo hakiwezi kuakhirishwa wala kuwahishwa kabla ya muda wake. Muda hauwezi kuzuiliwa wala kuwahishwa hata kidogo. Hakuna yeyote awezaye kuukimbia muda wa kifo.

Ndio maana wale wote wanaowajibikiwa kutekeleza ibada ya hijja wanatakiwa walifikirie sana jambo hili. Tunatakiwa kuacha upuuzaji na uvivu katika kuitekeleza ibada hii; kwa maana majuto baada ya kufa hayana faida. Kwa hali hiyo, waumini wenye uwezo wanatakiwa kutumia fursa ya mapema kabisa na wasighafilike katika kutekeleza wajibu wao. Vinginevyo onyo la Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) ni wenye kutisha na kuogofya sana:

"Kama mtu hakutekeleza hijjah yake baadaya kuwa na fursa na kuwa na mahitaji ya msingi kama vile kipandwa na mali, basi hakuna kitakamchozuia kufa akiwa kama Myahudi au Mkristo." (Tirmidhi, Hajj, 3)

Onyo hili kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w) linaelezea hasara ya wale wasiotekeleza faradhi ya hijja wakati wana uwezo wa kufanya hivyo. Hivyo, hasara iliyoje kwa Waislamu wenye uwezo

na wakawa wanaipuuza ibada hii!...

Hijjah ni faradhi inayotakiwa kutekelezwa mara moja katika umri wa mtu kwa wale wenye uwezo wa kufanya hivyo. Pia tumeusiwa kwenda kuhijji zaidi ya mara moja na pia ina thawabu nyingi. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) anasema:

"Kufanya hijjah (hijjah kubwa) na Umrah (hijjah ndogo) mara kwa mara hurefusha umri na kuongeza baraka na kuondoa dhambi kama ambavyo viriba huondoa kutu kwenye chuma." (Ahmad, III, 446-447)

Vilevile imeelezwa katika Hadith al-Qudsi:

"Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: Mja wangu asipokuja kwangu mara moja (yaani asipofanya hijja au umra) kila baada ya miaka minne, basi huyo ni fukara hata kama ana afya na mali." (Haythami, III, 206)

Kama ambavyo kuna swala au funga za sunna, vivyo hivyo kona hijja ya sunna. Hivyo, muumini anatakiwa kuwa makini dhidi ya ukosoaji wa kijinga unaotolewa na watu dhidi ya kutekeleza hijja za suna kwa kuwa hilo linaweza kumpelekea mtu kwenye ukafiri. Baadhi ya watu wanafikiri kuwa kufanya hijjah ya sunna ni kupoteza pesa. Mawazo hayo hutokana na ujinga mkubwa ambao hauna

msingi katika dini na hauna faida katika imani na ibada.

Ibada za sunna zimekuwepo tangu siku za mwanzo za Uislamu. Yafaa kuukumbuka mfano wa Imamu Abu Hanifa, ambapo alifanya hijja mara hamsini na tano katika uhai wake. Japokuwa alikuwa na wanafunzi wengi na majukumu mengi lakini alitumia moja ya tatu ya maisha yake katika hijjah. Jaribu kuvuta taswira ya ugumu uliokuwepo katika zama hizo kusafiri kwa ngamia kutoka Baghdad kwenda Makkah na Madina. Kutokana na ukweli kwamba marafiki wa Mwenyezi Mungu hawapati furaha mahala pengine zaidi ya mazingira matukufu ya maeneo haya, waliona kuwa ni hazina yenye thamani kumtembelea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kila walipopata fursa.

Ibada inayotekelezwa kwa dhati na usafi wa moyo humuwezesha mja kuwa karibu na Muumba. Amali hizo huongeza utambuzi na hisia ya moyo. Mwenyezi Mungu mtukufu huwa macho na masikio ya muumini hao. Kwa maneno mengine, macho, mawazo na fikra zao hugeuka ishara ya nuru kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

KUMTEGEMEA MWENYEZI MUNGU MTUKUFU NA KUJISALIMISHA KWAKE

Kutokana na utaratibu wake maalumu, Hij-

jah humpeleka mwanadamu kwenye utambuzi wa kiroho na kimaanawi. Ka'bah ni sehemu iliyojaa kumbukumbu za uaminifu na kujisalimisha kwa Nabii Ibrahimu (a.s) na familia yake mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Maneno ya imani, kujisalimisha na kuhiji yanapotajwa pamoja, mtu humkumbuka Nabii Ibrahimu (a.s) na mwanaye Nabii Ismail (a.s). Hijjah imegeuka kuwa amali ya watu wema, itakayoendelea kutekelezwa mpaka siku ya mwisho.

Neno la kiarabu *tawakkul* lina maana ya "ku* wa na imani, kutegemea na kuteua wakala." Katika istilahi ya Kisufi, neno hili lina maana kwamba mtu ambaye moyo wake umejaa upendo wa Mwenyezi Mungu humuamini na kumtegemea Mwenyezi Mungu pekee na kujilinda kwake. Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuuliza Musa kuhusu fimbo iliyokuwa mkononi mwake na kumuamuru kuwa "itupe"; kwa sababu ilikuwa inamzui Musa kumtegemea Mwenyezi Mungu.

Hili limeelezwa katika aya kadhaa:

"…Na juu ya Mwenyezi Mungu ndio wategemee Waumini." (Ibrahim 14; 11, al-Tawba 9; 51)

"…Na mtegemeeni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni Waumini." (al-Maida 5; 23)

"..Na anaye mtegemea Mwenyezi Mungu Yeye humtosha…" (al-Talaq 65; 3)

Imelezwa katika moja ya hadith za Mtume (s.a.w):

"Mkimtegemea Mwenyezi Mungu kikamilifu, mtapata baraka za Mwenyezi Mungu mfano wa ndege wanaoviacha viota vyao wakati wa asubuhi wakiwa na njaa na kurudi jioni wakiwa wameshiba." (Tirmidhi, Zuhd, 33)

Kumtegemea Mwenyezi Mungu haimaanishi kuacha kuchukua tahadhari na juhudi mbalimbali. Kinyume chake, ina maana ya kufanya kila liwezekanalo kufanyika na kisha ndio unajilinda kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwenyezi Mungu Mtukufu amelielezea hili katika Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

"…na shauriana nao katika mambo. Na ukisha kata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu…" (Ali- Imran 3: 159)

Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi na Msaidizi wa waumini duniani hapa na akhera pia. Mwenyezi Mungu anawatosha wale wote wanaomtegemea. Amani na utulivu wa kweli, wa mtu mmoja mmoja au jamii kwa ujumla, hupatikana kwa kumuelekea Yeye, kumuomba na kumtegemea Yeye tu.

Taslimiyyah ni neno la kiarabu lenye maana ya kujisalimisha. Neno hili asili yake ni neno «سَلَمَ" . Neno hili hutumika kuonesha utii kamili na kuyapokea matukio kama yalivyo. Na hivyo, jambo

hili huleta wokovu.

Katika moyo wa Ibrahim (a.s) hakuna nafasi ya kitu kingine chochote isipokuwa Mwenyezi Mungu. Ndio maana Mwenyezi Mungu Mtukufu alimtangaza Ibrahim kuwa ni rafiki Yake. Malaika wakauliza:

"Ewe Mola wetu! Ibrahim ana uhai, watoto na mali. Je anawezaje kuwa rafiki yako?"

Hapo Mwenyezi Mungu Mtukufu akawaletea mifano mitatu ya utii wa Ibrahim bila pingamizi. Mitihani hii mitatu na matokeo yake utakuwa mfano hai wa kuigwa na waumini hadi mwisho wa ulimwengu huu.

Pindi Ibrahim (a.s) alipotupwa kwenye moto malaika walikuja kwa lengo la kumsaidia. Lakini aliwaambia:

"Siwahitaji.Nani aliyeupa moto huu nguvu ya kuunguza?" Kisha akajilinda kwa Mola wake akisema:

"Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi ninayemtegemea, hakika Yeye ni Mlinzi bora." Alipotamka maneno hayo ya kujisalimisha Kwake, moto ulipewa amri kwamba:

"Ewe moto! Kuwa baridi na salama kwa Ibrahim!" (Al-Anbiya 21:69)

Nabii Ibrahim (a.s) aliichukulia mali yake kama kitu kisichokuwa na tahamani na aliitoa mali hiyo na kumpa Jibril (a.s) pindi Jibril alipolitaja jina Mwenyezi Mungu mara tatu.

Kwa mara nyingine tena, Nabii Ibrahim (a.s) alijaribiwa kwa kuambiwa amchinje mwanaye na akaushinda mtihani huo kwa mafanikio.

Utii ndiyo unyenyekevu wa kweli, kwa maana Mwenyezi Mungu Mtukufu hakubali waja Wake kukitegemea chengine kinyume Chake.

Kujisalimisha ni utii utokanao na upendo. Kutokana na utii wake na unyenyekevu wake, Mali ya Ibrahim, watoto wake na hata maisha yake havikumzuia kuelekea kwa Mola wake. Hijjah ni alama bora kabisa ya Ibarhim kumtegemea Mwenyezi Mungu na kujisalimisha kwake.

Ulimi wa Ibrahim (a.s) uligeuka kuwa mkalimani wa kile kilichokuwa moyoni mwake na daima alikuwa akisema:

"… nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu wote." (Al-Baqara 2: 131)

Hijjah, ambayo ni alama ya uaminifu na unyenyekevu wa Ibrahim (s.a) na Ismail (a.s) kwa Mwenyezi Mungu, ina maana ya kuacha sifa zote za kibinadamu na kuingia katika ulimwengu wa rehma na huruma. Ni kuwa mtiifu kwa kujiamini.

Hijja ni utiifu uliojaa upendo.

Hijja imetuonyesha kuwa kuondokana na dhambi kunawezekana tu kwa kutumia ibada inayotekelezwa kwa moyo uliojaa majuto, toba kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu na kumtegemea.

Waumini wanaotarajia kwenda kuhijji au kufanya umra hawana budi kuelewa maana ya kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu na kumtegemea. Hawana budi kufanya maandalizi ya mali na roho kwa ajili ya safari hiyo. Aya ifuatayo ilishuka kwa sababu baadhi ya watu wa Yemeni walikuwa wanasema "tunamtegemea Mwenyezi Mungu" bila kufanya maandalizi ya lazima kwa ajili ya hijjah yao:

"…Na jitengezeeni zawadi. Na hakika bora ya zawadi ni uchamungu…!" (al-Baqara 2:197)

Kama ilivyoelezwa katika aya hii, tunapokuwa kwenye ardhi tukufu ya hijjah tunahitaji kuwa na maandalizi ya kimaada na kiroho, ambayo ni muhimu zaidi. Hili linawezekana kwa yule mwenye moyo uliosalimika, mwenye uchamungu. Mojawapo ya matokeo ya maisha yenye kuongozwa na adabu na maadili sahihi ya Kiislamu ni kupata moyo wenye utambuzi na hisia unaoakisi ishara za uchamungu.

MUONGOZO WA KIROHO KWA AJILI YA HIJJA NA UMRAH YENYE KUKUBALIWA

Ufuatao ni muongozo unaomlazimu mtu kufuata kwa ajili ya hijjah au umrah yenye kukubaliwa na isiyokuwa na kasoro:

1. **Kuwa na nia ya dhati ya kufanya hijjah au Umrah na kuachana na mwenendo unaopingana na nia yake:**

Ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu na kunufaika na baraka Zake, yatupasa kuweka nia ya dhati ya kufanya hijjah na yatupasa kumuahidi Mwenyezi Mungu kuwa tutazitakasa nyoyo zetu na kuyaacha matamanio yetu ya kihayawani. Katika ardhi hizo tukufu, tunatakiwa kusahau miili yetu ya nje na kutoitikia matamanio ya nafsi zetu. Wale wenye kufanya hijja katika hali hiyo watapata rehma na Baraka za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hujaji wa aina hiyo anaweza pia kuwa mgeni katika pepo ya hekma na siri. Baada ya hatua hii ya kwanza, anatakiwa kufanya sehemu hizo tukufu yatupasa kusahau ubinadamu wetu na vilevile nafsi zetu. Wale wote wanaofanya hijjah katika hali hiyo watakuwa na yafuatayo:

2. **Unapovua mavazi ya kawaida ya kidunia ili kuvaa ihram (vazi maalumu la hijja), unatakiwa pia kuvua kila kitu ndani ya**

moyo wako na kumbakisha Mwenyezi Mungu pekee.

Miongoni mwa hekma za kumuahidi Mwenyezi Mungu na kutia nia ya dhati ya kutekeleza ibada yetu ya hijja ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ili kuondosha aina zote za matamanio ndani ya nyoyo zetu, kama vile tamaa ya mali, umaarufu na cheo. Tunapovua mavazi yetu ili kuvaa *ihram*, tunatakiwa pia kuziondosha hisia hizo nyoyoni mwetu na kuvaa vazi la uchamungu. Kwa sababu hiyo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kuwa:

"Hakika amefanikiwa aliye itakasa [nafsi yake]" (al-Shams 91: 9)

Unapokuwa katika ardhi hizi tukufu, unatakiwa kuacha kushughulika na mambo ya kidunia kama vile kuzurura sokoni kadiri iwezekanavyo. kujishughulisha na mambo kama hayo hudhoofisha mawasiliano ya moyo wake na ulimwengu wa kimaanawi na kukuingiza katika hali ya kughafilika. Unapoweka mkazo wako kwenye mambo na mahitaji hayo ya kidunia, inakuwa vigumu sana kunufaika na hali ya kiroho ya ardhi hizo tukufu.

Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alipoulizwa kuhusu kukaa Makkah hata baada ya kumaliza hijjah alisema:

"Makkah si sehemu ya kukaa. Baada ya kum-

aliza ibada na taratibu za hijjah kuna siku tatu tu za kukaa Makkah kwa wageni." (Ahmad, IV, 339)

Maneno haya yanaunga mkono tulichokieleza. Vile vile Umar (r.a) aliwausia mahujaji kurudi makwao mara baada ya kumaliza hijjah ili wasiathiri heshima wanayoupa mji wa Makkah.

Wakati wa hijja na Umrah, uelekeze moyo wako kwa Mola wa Kaabah na utafakari maana ya aya **"…Na Sisi tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingoni mwake…."** (Qaf 50:16)

Pia huna budi kutambua kuwa hakuna jambo linaloweza kufichika mbele ya Mwenyezi Mungu kama ilivyoelezewa katika aya ifuatayo: **"…na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake…"** (al-Anfal 8:24)

Kwa maneno mengine, unatakiwa kuachana na matamanio ya muda mfupi ya dunia hii na kujaribu kadiri uwezavyo kuufanya moyo wako ushughulike na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hii ni kwa sababu msingi wa hijjah ni:

3. Kutakasika kiroho na kimwili:

Wakati akielezea matokea ya amali na matendo mema yanayofanywa wakati wa hijja, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alibainisha malengo ya ibada hii tukufu kama ifuatavyo:

"Changanya hijja na umrah, kwa maana zina-

ondosha dhambi kama ambavyo viriba huondoa kutu kwenye chuma." (Nasai, Manasik, 6; Ibn Majah, Manasik, 3)

Umrah, au hijjah ndogo, ambayo inashauriwa ichanganywe na Hajj, ni ibada muhimu sana. Huzitakasa nyoyo za waumini na kuimarisha imani yao kwa Mwenyezi Mungu.

Tofauti na hijja, ambayo hufanyika katika kipindi cha siku maalumu za mwaka na kufanyika mara moja tu kwa mwaka, Umrah inawezekana kufanyika mara nyingi kadiri mtu awezavyo. Kwasababu ya faida zake, Umrah huitwa hijjah ndogo. Huna budi kuelewa vizuri maana ya ibada hii yenye faida na fadhila nyingi.

Umar ibn al-Khattab (r.a) anatwambia:

"Nilimuomba Mtume (s.a.w) ruhusa ya kufanya umra. Aliniruhusu na kuniambia:

"Ndugu yangu usinisahau katika maombi yako." (Tirmidhi, Daawat, 109/3562)

Umar (r.a) aliposikia maneno haya aliielezea furaha yake kama ifuatavyo:

"Maneno haya ya Mtume yalinifariji sana kiasi kwamba nisingefarijika hata kama ningepewa dunia yote hii." (Abu Dawud, Witr, 23/1498)

Mbali na faida zake nyingine, mfano huu pia

unaelezea kuwa uwezekano wa kukubaliwa dua na maombi wakati wa Umrah ni mkubwa zaidi kuliko wakati mwingine wowote ule. Hivyo dua na maombi ya kweli yanayoombwa wakati wa Umrah yana thawabu na malipo makubwa sana.

Umrah ambayo hufanyika baada ya Hajj, hususan katika kipindi cha mwezi wa Ramadhan ni nyenzo na njia ya kujitakasa kiroho. Kpenzi chetu, Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema kuwa: "Umrah wakati wa mwezi wa Ramadhan inatosha kuwa hijja yangu." (Tazama: Bukhari, Umrah, 4; Muslim, Hajj, 221)

Pindi hijja na Umra zinapofanywa kwa lengo la kupata thawabu kubwa, basi lazima yawepo mambo mengine muhimu ambayo hujaji anatakiwa kuwa makini nayeo, mambo hayo ni kama vile:

4. Kujiepusha na haramu na vitu vyenye kutia shaka, kuingia maeneo matakatifu kwa heshima kubwa, na kuzipa alama za kidini heshima stahili.

Hakika jambo la kwanza kabisa ni kuwa, matendo mema yote ya ibada yanatakiwa kufanywa kutokana na mapato halali; kwa sababu faida na manufaa ya kimaanawi ya ibada hupatikana tu kwa mwili uliostawi kutokana na chakula halali. Maneno yafuatayo kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w) ni muhimu sana katika suala hili:

"Mwenye kutembelea Nyumba hii (Kaabah) kwa kutumia vyanzo vya haramu atakuwa amemuasi Mwenyezi Mungu. Mtu huyu anapokusudia kufanya hijja, akachukua kipandwa chake, akaanza safari na kisha akasema: "Labbaik, Allahumma Labbaik! (Ewe Mwenyezi Mungu! Nimekuitika)," sauti kutoka mbinguni huita:

"La Labbayk walaa sa'dayk (hujaitikiwa), kwa sababu pato lako ni la haramu, chakula chako ni cha haramu, na kipandwa chako ni cha haramu. Rudi bila thawabu. Huzunika kwa maana utakutana na usichokipenda."

Lakini mtu mwenye kujiandaa na safari ya hijja kwa kutumia pato la halali, kapanda kipandwa chake na kusema "Labbaik, Allahumma Labbaik! (nimekuitikia Mola wangu nimekuitika)," sauti kutoka mbinguni huita:

"Labbaik wa sa'daik! Nimeiitikia wito wako, kwa maana kipandwa chako ni cha halali, mavazi yako ni ya halali, na chakula chako pia ni cha halali. Rudi nyumbani ukiwa na thawabu tele na bila dhambi. Furahi, kwa sababu utapata vitu utakavyovifurahia. " (Haythami, III, 209-210)

Kwa mujibu wa hadith hii, mwenye kwenda hijja na "*Labbaik*" kwa ulimi tu hatapata chochote katika safari yake zaidi ya maneno "*Laa Labbaik*."

Ndio maana pato la halali ni sharti la kwanza la hijjah. Kisha nia ya dhati hufuatia. Kila *Labbaik* au kifungu cha maneno "Ewe Mwenyezi Mungu! Nimekuitika" yanayotoka kinywani mwako yanatakiwa kuuchoma moyo wako kwa upendo na shauku. Sauti za *Labbaik* humweka mja karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu, lakini maneno matupu hayana faida yoyote kwa mja. Hii ndio wakati mjukuu wa Mtume, Hussain (r.a) alipokuwa akisoma maneno "*Labbaik,*" rangiyake ilikuwa ikibadilika kwa wasiwasi: "itakuwaje kama nikipata 'La Labbaik' kama jibu."

Vilevile kuna makatazo ambayo waumini wanatakiwa kujizuia nayo. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika Qur'an:

"Hija ni miezi maalumu. Na anaye kusudia kufanya Hija katika miezi hiyo, basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika Hija. Na kheri yoyote mnayo ifanya Mwenyezi Mungu anaijua. Na jitengezeeni zawadi. Na hakika bora ya zawadi ni uchamngu. Na nicheni Mimi, enyi wenye akili." (al-Baqara 2; 197)

Kwa muktadha huu, kumbuka kuwa mtu hutakiwi kuwa mbali tu na matamanio ya kihayawani kama vile uzinzi, udhalilishaji na kuzungumza kwa hasira wakati wa hijja, bali pia unat-

akiwa kuwa makini usiwaumize waja wa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu ya msongamano, daima mahujaji huwa katika hatari ya kuumizana. Ili kuiepuka hatari hii, unatakiwa kuwa makini sana, hususani wakati wa kuizunguka Ka'bah, na usijaribu kwenda uelekeo tofauti na ule wa watu wengine.

Pia unatakiwa kuwa makini kuhusu mipaka ya staha ndani ya viwanja vya Ka'bah au kwenye ngazi za hotelini ambapo kuna mwingiliano wa wanawake na wanaume. Unatakiwa kuzingatia utaratibu na utu wakati wa kuingia na kutoka msikitini. Katika ardhi hii takatifu unatakiwa kukumbuka kuwa hairuhusiwi hata kuchuma jani. Kila ulifanyalo laweza kukuleta karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu na jitahidi sana kuufanya ukali na matendo yako mabaya yabadilike kuwa upendo, huruma, upole na umaridadi. Usisahau kuwa kama ilivyo kwa amali njema, dhambi na matendo mabaya nayo hulipwa.[2]

Umakini huo ni katika mambo ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alisisitiza mno katika maisha yake matukufu. Siku moja Mtume (s.a.w) alimwambia Umar (r.a):

"Ewe Umar! Wewe ni mtu mwenye nguvu.

2. Tazama: Qasimi, M. Jamal al-Din, Zubdat al-Ihya, Istanbul, 1999, uk. 94

Usiwasukume watu wala kuwabana walio dhaifu ili ufike karibu na jiwe jeusi. Usisumbue wala usisumbuliwe! Kama msikiti upo mtupu waweza kwenda na kulibusu, vinginevyo fanya ishara ya kuligusa na kulibusu kwa mkono wako. Pita tu ukisoma takbir[3] *na tahlil*[4]*."* (Haythami, III, 241; Ahmad, I, 28)

Kama ishara ya utambuzi huu, Umar (r.a) aliiambia Ka'bah akisema:

"Utukufu wako ulioje (ewe Ka'bah)! Adhama yako iliyoje! Lakini mbele ya Mwenyezi Mungu heshima ya muumini wa kweli ni kubwa kuliko yako. " (Tirmidhi, Birr, 85)

Kwa hiyo muumini anatakiwa awe makini sana asije asimuumize yeyote katika viwanja hivyo vitukufu. Vile vile unatakiwa kuchunga adabu na mwenendo wako wa nje na ndani. Dhumuni la hijjah ni kuonyesha heshima kwenye sehemu hizo tukufu na kuibadilisha hali yako ya kiroho kwa kuyakumbuka matukio yaliyotokea huko. Imeelezewa katika aya moja ya Qur'an kuwa:

"…na anayetukuza ibada (ishara) za Mwenyezi Mungu, basi hayo ni katika unyenyekevu wa nyoyo." (al-Hajj 22: 32)

3. Allahu akbar , yaani Allah ni Mkubwa
4. La ilaha illallah, yaani hakuna Mungu apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah

Kwa hiyo swala, misikiti, Qur'an tukufu, adhana, Ka'bah tukufu, vilima vya Safa na Marwa, na vitu vingine vitukufu vyote ni alama za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Muumini anatakiwa kuziheshimu sana alama hizi wakati wa hijjah.

Epuka mwenendo mbaya kama vile kukaa au kulala ukiwa umenyoosha miguu kuielekeza upande wa kaabah, kuzungumza mambo yasiyo na maana na kusoma Qur'an katika njia isiyo sahihi na kutupa sakafuni.

Vile vile, tunapokuwa katika ardhi hizo tukufu, yatupasa kufanya juhudi za kuwasaidia wenye shida. Tunatakiwa kushiriki kutatua shida za wasafiri, wagonjwa, wasiokuwa na uwezo wa kiuchumi, na wale waliofiwa. Hiyo ni ishara ya sifa adhimu kama vile, huruma, upole na uungwana, ambazo moyo wa muumini unatakiwa kuwa nazo. Vilevile tunatakiwa tusiuvunje moyo ambao ni mahali panapotazamwa na Mwenyezi Mungu, bali tuuimarishe na kuufanya kuwa wenye kumkumbuka daima.

Katika tungo zifutazo, Jalal al-Din Rumi (q.s) anaelezea kwa uzuri kabisa kuwa undani na uhalisia wa hijja unaweza tu kueleweka kupitia moyo wenye utambuzi, hisia na ulaini:

"Bayazíd, shaykh wa ummah, alikuwa akifanya haraka ya kwenda Makkah kuhiji na kufanya

umrah. Katika kila mji aendao alimtafuta kwanza mtu anayeheshimika (walii). Alizunguka akiuliza, "Je kuna mtu yeyote kwenye mji huu mwenye utambuzi wa kiroho?" Alikuwa akitambua umuhimu wa kuwatafuta marafiki wa Mwenyezi Mungu kwa kuwa Mwenyezi Mungu amesema,

"… Waulizeni wenye ilimu ikiwa nyinyi hamjui" (al-Anbiya 21; 7)

Hata Musa (a.s) aliamuriwa amtembelee Khizr aliyekuwa na elimu ya siri kubwa. Hivyo, Bayazíd, akiwa katika safari yake (kuitembelea Ka'ba), alitumia muda mwingi kumtafuta Khizr wa zama zake. Alimuona mzee mmoja aliyekuwa na mwili uliopinda kama mwezi mchanga; aliona taadhima na maneno ya watu watakatifu; macho yake hayakuwa na uoni na moyo wake uliangaza kama jua…

Bayazíd alikaa chini mbele yake na kumjulia hali; aligundua kuwa alikuwa darwesh na mwenye familia. Yule mzee akasema, "Unakwenda wapi, Ewe Bayazíd? Unaupeleka wapi mwili wako katika ardhi hii ya ugenini?"

Bayazíd akajibu, "ninataka kwenda kuitembelea Kaabah wakati wa kupambazuka." "Eh, " akapiga kelele na kusema, "je umebeba nini kama maandalizi na ruzuku ya safari?"

"Nina dirham mia mbili za fedha, "akasema; "tazama, zimefungwa kwenye joho langu."

Yule mzee akasema:

"Gawa sehemu ya fedha hizo kwa masikini na mafukara kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Ingia ndani ya nyoyo zao na upate dua zao ili anga ya moyo wako ipate kusafika. Jipatie maisha yasiyo na kikomo. Ifanye roho yako ianze kuhiji kabla. Kisha endelea na hijja yako ukiwa na moyo huu wenye hisia ya ndani na utambuzi.

Kwa sababu Ka'bah ni nyumba ya Birr (wema) ya Mwenyezi Mungu (yaani ni mahali pa rehma inayompeleka mja kwenye ukamilifu wa imani na kumuweka karibu zaidi na Mwenyezi Mungu). Ni nyumba ambayo ni faradhi kuitembelea kama mojawapo ya shuruti za Uislamu. Lakini moyo wa mwanadamu ni hazina ya siri mbalimbali.

Ka'bah ni nyumba ya Ibrahim mwana wa Azar; wakati moyo ni kituo maalumu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kama una utambuzi, basi izunguke Ka'bah ya moyo. Roho ndio maana halisi ya Ka'bah, ambayo unadhani imejengwa kwa mchanga na mawe. (Kwa maneno mengine moyo wako huzidi kumkurubia Mwenyezi Mungu kwa njia ya Ka'bah.)

Mwenyezi Mungu amekuamuru kuizunguka Ka'bah ya kimaada ili uifikie Kaabah iliyotakasika na kusafika kwa moyo.

Tambua hili kuwa hijjah ni ibada ya faradhi ambayo lazima uitekeleze; lakini pia unatakiwa utambue kuwa kuumiza na kuuvunja moyo ambao ni mahali panapotazamwa na Mwenyezi Mungu, dhambi zako hazitaondoshwa na safari yako hata kama utasafiri kwa miguu.

Bayazíd aliyasikiliza maneno yale ya siri na kuyaweka sikioni mwake kama pete ya dhahabu. Kupitia kwa bwana yule mzee, imani ya Bayazíd ilipata ongezeko (la kipwa cha kiroho): utambuzi mwishowe ukapatikana." (Mathnawi, II, aya: 2218-2251)

Rumi, anayeziongoza nyoyo kwenye njia iliyo-nyooka kwa mfano huu mzuri na mingine mingi, anawaambia wale wanaopenda kutembelea ardhi tukufu:

"Wakati wa hijjah ukifika, nendeni na kuizun-guka Ka'bah. Mkienda huko kwa nia hii, mnaweza kuuona uhalisia wa Makkah."

Sababu ya Rumi kutoa mfano huu maalumu ni kwa kuwa hijjah ni tendo muhimu mno la ibada. Ndiyo unatakiwa kufunga safari ya hijja baada ya kufanya maandalizi ya kiroho.

Hijja na umrah inayofanywa bila hisia hizi hazitaleta matokeo yanayotarajiwa. Ndiyo maana hijja zote zinatakiwa kufanyika kwa moyo wenye hisia kwamba ibada hiiinatakiwa igeuke kuwa

amali bora yenye kustahili kupata sehemu ya jamala ya malaika. Ndiyo maana mahujaji wakiwa wamevaa ihram hawaruhusiwi kuwinda, kuchuma majani, au kuchomoa hata unywele mmoja. Wale wote wanaovaa ihram hutambua ulazima wa kujiepusha na vitu vya haramu na vile vya kutiliwa shaka kwa kukaa mbali na vitu vya halali wakati wa hija kwa kipindi cha muda maalumu. Wanatambua umuhimu wa kuwa na huruma, upole na wema kwa viumbe, na hususan kutouvunja moyo wowote kutokana na heshima waliyo nayo kwa Muumba wao.

Jukumu muhimu zaidi katika hijja na umrah wakati wa hijja na Umrah ni kutumia pumzi na muda wetu wenye kikomo hapa ardhini kufanya matendo yenye thamani sana. Daima tunatakiwa kuepuka kupoteza muda wetu kutafuta kasoro na mapungufu ya watu wengine, jambo ambalo halituhusu kabisa. Hali yetu pia wakati wa hijja inatakiwa kuakisi kiwango cha utambuzi wa nyoyo zetu na ukubwa wa hali yetu ya kiroho.

Waumini hawatakiwi kuwadharau, kuwachukia na kuwakaripia ndugu zao katika Uislamu; kwa sababu, huwezi kujua mwenzako ana daraja gani, hususan unapokuwa katika ardhi tukufu. Macho ya mwanadamu hayawezi kujua kilichomo ndani ya moyo wa mtu bali Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye.

Kisa kifuatacho cha Khalid al-Baghdadi (q.s) kabla ya kujiunga na njia ya Usufi ni kisa muhimu sana kuhusu suala hili:

Siku moja Khalid al-Baghdadi (q.s) alifunga safari kwenda kufanya ibada ya hijja na kufika Madina. Huko akakutana na mtu mwenye muonekano wa haiba na wema. Khalid al-Baghdadi alivutiwa sana na rafiki huyu wa Mwenyezi Mungu kutoka Yemen na akaanza kuomba ushauri kutoka kwake kama mtu mjinga amulizavyo maswali msomi. Yule bwana akajibu:

"Ewe Khalid! Ukifika Makkah, ukimuona mtu anafanya jambo unalodhani kuwa halifai kwenye Ka'bah, usiwe mwepesi kumuhukumu na kufikia kwenye hitimisho baya. Yaepusehe macho na moyo wako kudadisi hali za watu. Shughulika na kuupamba ulimwengu wako wa ndani."

Japokuwa maneno haya yalionekana kama onyo jepesi kwa Khalid al-Baghdadi (q.s), kiuhalisi kulikuwa na ishara za mawasiliano ya siri baina yake na mtu yule ambaye angempitisha katika vituo vya kimaanawi.

Khalid al-Baghdadi alipofika Makkah, alisahau onyo alilopewa na mzee yule kwa sababu ya mazingira ya kiroho ya Makkah. Siku ya Ijumaa, alimwona darweshi mmoja wa ajabu na aliyekuwa na muonekano wa hovyohovyo, na ambaye ali-

kuwa ameugeuza mgongo upande wa Kaaba na akawa akimtazama. Khalid al-Baghdadi akafikiri:

"Mtu gani huyu aliyeghafilika! Ameigeuzia mgongo Ka'bah. Hautambui utukufu wa mahali hapa penye Baraka."

Hapo bwana huyo aliyekuwa akitazamana na Khalid, akamwambia:

"Ewe Khalid! Hujui kuwa kumuheshimu muumini mwenzako ni bora kuliko kuiheshimu Ka'bah? Kwa sababu moyo ndio mahali panapotazamwa na mwenyezi Mungu. Moyo safi na imara ndiyo nyumba ya Mwenyezi Mungu. Kumbuka wosia uliopewa na mtu mwema kule Madina…"

Hapo Khalid al-Baghdadi (q.s) akatambua makosa yake na kuelewa kuwa mtu huyu ni walii mkubwa. Akamtaka radhi na kumuomba:

"Ewe mtu mwema! Tafadhali nisaidie na unikubalie kuwa mwanafunzi wako." Darweshi yule mwenye maajabu akatazama angani na kisha akajibu:

"Mafunzo yako hutayapata kwangu. Utapata ukamilifu chini ya usimamizi wa Abdullah Pir-i Dahlawi kutoka katika mji wa Delhi huko India. Mwenyezi Mungu akupe mafanikio! …"

Katika muktadha huu, ningependa pia kusimulia wosia ufuatao kutoka kwa baba yangu Musa Topbash (q.s):

"Ufuatao ni wosia wangu kwa wanaokwenda hijjah: daima jitahidini kuwa na heshima. Shughulika na ulimwengu wako wa ndani. Usipoteze muda wako kwa vitu visivyokuwa na faida. Jaribuni kufaidika na ishara za kimaanawi na kiroho zinazopatikana katika ardhi hizi takatifu.

Ni dhahiri kuwa mtu akienda hijjah hali yake ya kiroho huimarika sana. Mara nyingi wale wanaotenda amali njema na kutoa sadaka wanatokana na wale wanaokwenda kuhiji mara kwa mara. Kutokana na maajabu ya kiroho ya hijja, mtu huimarisha sifa mbalimbali kama vile ukarimu, huruma na upole. Mikono na nyoyo za watu hao huwa wazi; na hutoa sadaka kwa hiari katika Baraka walizopewa na Mwenyezi Mungu kwa ajili Yake Mwenyezi Mungu."[5]

Kama ilivyoelezwa katika aya:

"Kabisa hamtafikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyo vipenda. Na kitu chochote mnacho kitoa basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua." (Al-i Imran, 3:92) hivyo, jambo muhimu ni:

5. Kuyatoa sadaka matakwa yako kwa ajili ya radhi za Mwenyezi Mungu:

Lengo halisi la kuchinja mnyama wakati

5. Topbaş, Musa, Allâh Dostunun Dünyâsından, İstanbul, 1999, uk. 112.

wakati wa hijjah ni kukumbuka jinsi Nabii Ibrahim (a.s) na mwanaye Ismail (a.s) walivyojisalimisha mbele ya Mwenyezi Mungu, kufaidika na hekma ya Mwenyezi Mungu iliyo ndani ya kisa chao kuufanya moyo utambue ulazima wa kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa usafi wa moyo na kwa kumcha. Kwa maneno mengine, unatakiwa kuwa katika hali kama ya wale wanaweza kuzivua roho zao kutoka katika miili yao ya kidunia na wale wanahisi kuwa hawana roho kabisa, kujisalimisha kikamilifu mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kuwa tayari kuunguzwa ndani ya upendo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an Tukufu:

"Nyama zao hazimfikii Mwenyezi Mungu wala damu zao, lakini unamfikia uchamngu wenu…" (al-Hajj 22; 37)

Hivyo, tunapochinja tunatakiwa kutafakari jinsi Ibrahimu (a.s) alivyomtoa sadaka mwanaye na mwanaye Ismail (a.s) akautoa kwa hiari kabisa uhai wake. Tunatakiwa kutafakari ni kwa kiwango gani tunaweza kuyatoa sadaka maisha yetu na mali zetu, na ni kwa kiwango gani tunaendana na sifa za waumini zilizotajwa katika aya hii isemayo: **"Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwa kuwa wao watapata Pepo.** (al-Tawba 9; 111) Ili tuweze kutoa dhabihu hizo kuna sharti tunalotakiwa kulitimiza:

6. Kumpiga shetani na kuzipiga mawe naf si zetu:

Kama tulivyoeleza hapo mwanzo, kumpiga mawe shetani kunaanza na kumpiga mawe Shetani aliye ndani mwetu. Kumpiga mawe shetani ni kukumbuka jinsi Nabii Ibrahimu (a.s), Ismail (a.s), na Hajar walivyompiga mawe shetani na kumfukuza kwa sababu alitaka kuyumbisha imani yao.

Daima tunatakiwa kuzihoji na kuziuliza nafsi zetu ni kwa kiwango gani tunaweza kuzipiga mawe wasiwasi zetu, shaka zetu na makosa yetu; ni mafunzo mangapi tunaweza kuyapata kutoka katika ikhlasi na unyoofu wa Ibrahimu, Ismail na Hajar pindi walipompiga mawe shetani; na ni kwa kiwango gani misimamo yao inatuathiri kiroho.

Hali na kiwango cha kiroho ambacho mja anatumaini kukifikia ni:

7. Kuwa katika hali endelevu ya kumuomba na kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu:

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an:

"…Na mtakapomiminika kutoka A'rafat mtajeni Mwenyezi Mungu penye Masha'ril Haram. Na mkumbukeni kama alivyo kuongoeni, japokuwa zamani mlikuwa miongoni mwa walio potea." (al- Baqara 2; 198)

“Na mkishatimiza ibada zenu basi mtajeni Mwenyezi Mungu kama mlivyokuwa mkiwataja baba zenu au mtajeni zaidi. Na wapo baadhi ya watu wanao sema: Mola wetu Mlezi, tupe dunia-ani! Naye katika Akhera hana sehemu yoyote. ”
(al-Baqara 2; 200)

Hakika, *talbiya*[6], ambayo imeamriwa kurudiwarudiwa wakati wa hijjah, inatufundisha kuwa katika hali endelevu ya kufanya dua na kumtaja Mwenyezi Mungu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) anasema:

“Hakuna muumini asomaye talbiya halafu miti, miamba, ardhi na vinavyomzunguka vikaacha kushiriki katika talbiyah yake. Huendelea kushiriki (katika talbiya yake) hadi mwisho wa ulimwengu, kulia na kushoto.” (Tirmidhi, Hajj, 14/828)

Talbiyah ni muhimu sana katika kutengeneza hali ya dhikri na maombi moyoni kiasi kwamba imeamriwa kusomwa na kufanywa kwa sauti ilhali matendo mengine ya ibada hufanywa kimya kimya. Kwa njia hii muumini hujishughulisha yeye na walio karibu naye katika kumdhukuru na kumuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) anas-

6. “Labbaik Allahumma Labbaik Labbaika la sharika laka labbaik inna’l hamda wa’l ni’mata laka wa’l mulk la sharika laka.”

ema katika moja ya maneno yake:

"Jibril alinijia na kuniamuru niwaamuru maswahaba wangu na watu walio pamoja nami kupaza sauti zao katika talbiyah." (Abu Dawud, Manasiq, 26/1814)

Katika maneno mengine, Mtukufu Mtume wetu (s.a.w) alitueleza jinsi ya kuongea ili kudumisha hali endeleve ya kumdhukuru na kumuomba Mwenyezi Mungu katika ardhi hizo takatifu:

"Kuzunguka Ka'bah ni sawa na kufanya ibada swala isipokuwa unaweza kuongea wakati wa kuizunguka Ka'bah. Kwa hiyo yeyote atakaezungumza wakati wa kuizunguka Ka'bah yampasa kuzungumza kuhusu mambo mema." (Tirmidhi, Hajj, 112)

Kwa kufuata misingi ambayo nimeshaibainisha, tunaweza kutarajia kufikia hatua ya:

8. Nafsi zetu kuonja ladha ya msamaha, neema na thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu:

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) anasema,

"Umrah hufuta dhambi zilizotangulia (baina yake na umra iliyopita). Na malipo ya Hijjah iliyokubaliwa na Mwenyezi Mungu ni peponi." (Bukhari, Umrah, 1)

Tamaa ya kila muumini anayefika kwenye ardhi hizi tukufu inatakiwa iwe ni kutekeleza wajibu wake kikamilifu na kustahili kuwa miongoni mwa wale wanaorudi nyumbani wakiwa hawana dhambi kabisa kama siku waliyozaliwa. Katika hili, Abu Hurayra (r.a) anasimulia kuwa Mtukufu Mtume (s.a.w) alisema:

"Atakayezuru Nyumba hii (Ka'bah) (kw nia ya kufanya ibada ya hijjah), na akawa hakuongea mambo machafu wala kufanya maovu, atarudi akiwa hana dhambi kama siku ya kwanza aliyozaliwa na mama yake." (Muslim, Hajj, 438)

Habari hizi njema ni kwa wale wote wanaofanya hijjah inayokubaliwa, au hijja iliyojaa wema na tunu kuanzia mwanzo mpaka mwisho.

Kama ilivyosisitizwa katika baadhi ya maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w), dhambi zote, isipokuwa zile za **"kukiuka haki za binadamu"** husamehewa baada ya kutekeleza hijjah yenye kukubaliwa. Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye Mmiliki wa msamaha, lakini haki za wanadamu zimeachwa kwa ajili ya akhera ili zishughulikiwe.

Lakini mtu asielewe vibaya maana ya habari hizi njema kuhusu msamaha huo wa jumla; kwa sababu hatuna habari iwapo swala, funga na zaka ambazo hazikutekelezwa zinaweza kuwekwa chini ya orodha ya madhambi yatakayosamehewa. Muu-

mini hana budi kujitahidi kutekeleza matendo hayo ya wajibu mpaka mwisho wa uhai wake. Kuna viwango viwili vya uwajibikaji wa muumini kwa kutotekeleza ibada zake:

1. Kuhesabiwa kwa kutozitekeleza

2. Na hata akitekeleza baada ya muda unaotakiwa, bado atawajibika kwa kutozitekeleza kwa wakati unaotakiwa.

Hata kama Mwenyezi Mungu mtukufu akitusamehe kwa hilo la pili, bado tutawajibika kwa yale tuliyoshindwa kutimiza. Ndio maana yampasa mtu kuyatekeleza matendo yake ya wajibu hata baada ya muda wake kupita. Ama kuhusu Zaka, yatupasa pia kuhesabu mfumuko wa bei na kuongeza hesabu yake kwenye deni. Pamoja na hayo, ni lazima kuomba msamaha wa Mwenyezi Mungu kwa kutozitekeleza kwa wakati.

Ndio maana wale wanaokwenda kuhiji hushauriwa kulipa madeni yao, kama yapo, kuomba msamaha kwa zile haki zilizokiukwa na kutekeleza swala, funga na kutoa Zaka ambazo hawakuzitimiza haraka iwezekanavyo. Tunapotegemea msamaha wa jumla unatokana na hijja, hatutakiwi kupuuza na kulegea katika kutekeleza wajibu wetu na kukiuka haki za wengine. Yatupasa kufanya kila tunaloweza na kama kuna matendo ya wajibu yaliyoachwa baada ya hapo, basi tunaweza kuomba

msamaha kwa Mola wetu na kuomba huruma Yake.

Alama ya hijja iliyokubaliwa ni pale **hujaji anapodumisha usafi wa kiroho alioupata wakati wa hijja na kukaakwenye njia iliyonyooka baada ya hijja yake.** Muumini hatakiwi kuonesha udhaifu katika kutekeleza majukumu yake kwa kutegemea eti atasamehewa kutokana na hijja yake. Hatakiwi kusahau kuwa ulimwengu huu ni mahali pa mitihani na majaribio. Kama ilivyoelezwa katika mojawapo ya maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w), kuna watu ambao hutenda amali za watu wa Peponi ikabaki hatua moja kati yake na Pepo, kisha akafanya matendo ya watu wa Motoni akaingia motoni.[7] Kwa bahati mbaya historia imejaa mifano ya watu hao wanaoteleza. Vivyo hivyo, muumini anatakiwa kuishi baina ya hali ya matumaini na wasiwasi na kuitumia aya isemayo "**Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini."** (al-Hijr 15: 99) kama kanuni ya maisha yake.

Hijjah inayotekelezwa kikamilifu au Hajj al-Mabrur, sio tu huleta habari njema kwenye maisha ya hujaji kuhusu msamaha wa jumla bali pia

7. Tazama: Bukhari, Qadar, 1

humpa sifa na tabia adhimu kama vile utambuzi wa kuwa na hisa ya kuwajibika, kusamehe, kuuweka mwili na moyo katika hali ya usafi muda wote, undugu wa Kiislamu, kutambua ukweli wa uchamungu ndiyo kipimo pekee cha ubora katika Uislamu, hisia ya kuchuma pato la halali, kumtegemea Mwenyezi Mungu, kujisalimisha kwake na usafi wa moyo (iklas). Haya ni baadhi ya malipo na manufaa ya hijja katika maisha haya na kesho Akhera.

Malipo na manufaa makubwa kabisa ya hijja ni kuwa, kwanza, hutufanya tupate radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Vile vile huongeza upendo baina ya waumini.

Hijja hufanyika katika mazingira matukufu na adhimu kabisa ambayo rehma za Allah zisizokuwa na kikomo hujionesha, na waumini, ambao hupata msamaha kwa rehma hiyo ya Mwenyezi Mungu huungana pamoja katika msisimko wa imani. Waumini wengi kutoka nchi mbalimbali, wanaotoka katika mazingira, rangi, lugha, desturi na mitindo tofauti ya maisha, huonesha mandhari ya ajabu ya umoja kuizunguka Kaabah. Upendo na hisia za wema na undugu huwafanya waumini wasahau tofauti za kimwili na za kijamaa baina yao. Hisia hizo huwageuza waumini kuwa moyo mmoja wenye mapigo.

Waumini hujionea uzuri wa undugu katika amani na utulivu wa umoja ulio ndani ya nyoyo zao.

Hivyo, hijja sio tu kwamba ni moja ya nguzo za Uislamu, bali pia ni kitu kinachoimarisha vipengele vya kijamii na kisiasa vya dini hii tukufu. Hijja husimama mbele yetu kama mnara mkubwa wa tabia ya umoja wa Kiislamu duniani.

KUZURU MADINA

Sehemu aliyopumzika Mjumbe wa Mwenyezi Mungu mjini Madina, ambayo mahujaji huitembelea ima kabla au baada ya hija, kiroho ni sehemu muhimu sana kwa waumini. Huko, nyoyo za waumini huhisi upendo wa Mwenyezi Mungu. Ndio maana tunapotembea na kuvuta hewa ya Madina, tunatakiwa kukumbuka na kutafakari kuhusu matendo na hewa aliyovuta Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Tunapolitembelea kaburi lake, tunataraji kujawa na hali yake ya kiroho na hatutakiwi kusahau kuwa mahali hapo ndiyo mapumziko ya mwisho ya kito chenye thamani zaidi ulimwenguni. Yatupasa kuonyesha heshima kubwa na msisimko mkubwa wa kuwa miongoni mwa umma wake.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alisema kuwa:

"…eneo lililopo baina ya vilima viwili vya Madi-

na nimelitangaza kuwa eneo takatifu kama Ibrahim (a.s) alivyoitangaza Makkah kuwa eneo takatifu na kuiombea…" (Bukhari, Fada'il al-Madina, 6; Muslim, Hajj, 462)

Tunatakiwa tumpende Mtume sana kuliko nafsi zetu, mali zetu, kuliko watoto wetu na hata kuliko chochote kile tulichonacho; kwa sababu ni mtu pekee ambaye Mwenyezi Mungu Mtukufu amemsifu kwa cheo cha "Habibi au kipenzi changu" na akawaamrisha waumini wampende. Katika muktadha huu, Qadi Iyad (a.r) alitafsiri aya ifuatayo:

"Sema:Ikiwa baba zenu na wenenu na ndugu zenu na wake zenu na jamaa zenu na mali mlizozichuma na biashara mnazoogopa kuharibika na majumba mnayoyapenda ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na jihadi katika njia yake basi ngojeeni Mwenyezi Mungu alete amri yake na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wapotofu." (al-Tawba 9: 24) kama ifuatavyo:

"Mwenyezi Mungu ameuamrisha ummah wa Mtume Muhammad kumpenda yeye mwenyewe pamoja na mjumbe Wake."

Upendo wa kitu husambaa na kuathiriwa na kila kitu kinachohusiana nacho. Kwa mfano, kinachoufanya mlima wa Uhud kuwa tofauti na

upendwe zaidi kuliko milima mingine duniani ni kwa sababu Mtukufu Mtume (s.a.w) aliupa upendo maalumu. Ndiyo maana mtu anapokuja Madina anatakiwa autazame Mlima Uhud kwa upendo. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alisema kuwa: *"Uhud inatupenda nasi lazima tunaipenda pia."* (Bukhari, Jihad, 71)

Kilichoufanya mji wa Madina kupendwa zaidi na waumini, japokuwa kabla ya hijra ulikuwa ukijulikana kama Yathrib, ni kutokana na uhusiano wake na Mtukufu Mtume (s.a.w) na kumbukumbu zake muhimu zinazopatikana huko. Waumini wanaupenda sana mji huu kwa sababu unawakumbusha kuhusu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) kila jina lake linapotajwa.

Vile vile ukimpenda Mwenyezi Mungu ni lazima umpende pia Mtume wake na kumtii. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuamrisha katika Kitabu Chake Kitukufu:

"Sema (ewe Muhammad!): ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi Mwenyezi Mungu atakupendeni... " (Al-I Imran 3; 31)

Kufanya juhudi za kumfuata na kumpenda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) hutupatia heshima ya kuwa miongoni mwa waja wanaopendwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Maswaha-

ba wa Mtume (s.a.w) walimsikiliza sana ili wapate kuwa karibu na ukweli wake na kunufaika na hali yake ya kimaanawi na ya kiroho. Kwa sababu hiyo, wakapata Baraka zisizokuwa na kikomo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ndiyo maana tiba mujarabu ya maradhi ya nyoyo zetu zilizoghafilika ni kumpenda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na **"kumtii na kuzifuata sunnah zake."**

Hakuna kinachotakiwa kutangulizwa mbele ya upendo wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w). Si nyumba, familia zetu, watoto wetu, kazi zetu wala majukumu yetu!

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alitumia maisha yake yote kuwapenda wafuasi wake, akiwalilia kwa kusema: "ummah wangu, ummah wangu". Aliwalinda kama mama anavyowalinda wanawe. Siku moja Mtukufu Mtume (s.a.w) aliwaambia maswahaba zake:

"Angalieni! Mimi ni mlizi wenu kipindi cha uhai wangu na baada ya uhai wangu, nitaendelea kusema nikiwa kaburini "ummah wangu , ummah wangu …" mpaka itakapopulizwa baragumu la kwanza la siku ya hukumu…" (Ali al-Muttaqi, Kanzu'l Ummal, juz. 14, uk. 414)

Mtukufu Mtume (s.a.w) alienda kwa Mola wake akirudia maneno haya *"ummah wangu, ummah wangu …"* Wakati akivuta pumzi yake

ya mwisho, alikuwa akieleza upendo, huruma na upole aliokuwa nao kwetu akisema:

"Nitawasubiri kwenye bwawa langu la Kawthar…"

Kwa mukhtasari, kama ilivyoelezewa katika Qur'an Tukufu:

"Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe: yanamhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni sana, kwa waumini ni mpole na mwenye huruma." (Al-Tawba 9; 128) Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alitufikiria sisi katika kilio chake, kicheko chake, huzuni na furaha yake, na katika ibada zake na maombi yake. Hata katika nyakati maalumu kama vile safari ya Miraj hakutusahau na alituhangaikia pia…

Alikuwa bahari kubwa ya rehma kiasi kwamba, kwa sababu yake, Mwenyezi Mungu hakuwateremshia majanga na masaibu watu wa Makkah hata walipomfanyia uonevu, kumkandamiza kumkana na kumuasi. Ni kwa sababu Mtume alikuwa akiishi miongoni mwao ndio maana waliachwa. Mwenyezi Mungu Mtukufu amelielezea hili kama ifuatavyo:

"Na Mwenyezi Mungu hakuwa wa kuwaadhibu nawe umo pamoja nao. " (al-Anfal 8:33)

Lakini hali ilibadilika baada ya Mtukufu Mtume (s.a.wikie) kuhama kutoka Makkah kwenda Madina. Majanga kutoka mbinguni yakaanza kutumwa kwa makafiri wa Makkah. Milipuko ya ukame na njaa ikatokea. Watu wa Makkah walipoangalia angani walihisi kizunguzungu kwa njaa kali.

Mwenyezi Mungu Mtukufu hatawaadhibu wale waliobeba upendo wa Mtume wake (s.a.w) ndani ya nyoyo zao. Mwenyezi Mungu atawezaje kuwaadhibu wale wote wanaompenda Mtume na kufuata sunnah zake katika maisha yao yote hali ya kuwa hakuwaadhibu makafiri kipindi walichokuwa wakiishi na Mtume Wake? Kwa upande mwingine, wale wasiokuwa na jua hili la uongofu ndani ya nyoyo zao hawataweza kuepuka adhabu ya Mwenyezi Mungu.

Kulipa upendo wake kwa kumpenda ni jukumu la awali kabisa kwa wale ambao wamepewa heshima ya kuwa katika umma wa sultani huyu wa mitume (s.a.w), ambaye daima aliwaweka waumini ndani ya maneno yake na ndani ya moyo wake.

Lakini kumpenda Mtukufu Mtume (s.a.w) haina maana ya kusema tu au kufikiria kuwa yuko moyoni mwake. Bali kutoknana na kanuni isemayo “wale wanampenda mtu huiga kile kinachopendwa na mpendwa wao na daima hum-

kumbuka," wale wanaompenda Mtukufu Mtume (s.a.w) wanatakiwa kuakisi na kuonesha Sunnah zake katika kila kipengele cha maisha yao. Waumini pia wanatakiwa kumuombea Baraka na rehma Mtukufu Mtume (s.a.w) na kumtolea salamu.

Kwa mujibu wa Imam Malik (a.r), kwa kuwa Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa na daraja ya juu kabisa mbele ya Mwenyezi Mungu, mahali lilipo kaburi lake mjini Madina linatakiwa kuchukuliwa kuwa eneo takatifu zaidi kuliko eneo ilipo Kaabah; kwa sababu ulimwengu wote uliumbwa kwa sababu ya upendo na kwa ajili ya Mtukufu Mtume (s.a.w).

Vile vile Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w), katika mojawapo ya maneno yake, alisema:

"Atakaenitembelea baada ya mauti yangu ni kama amenitembelea wakati wa uhai wangu." (Daraqutni, Sunan, II, 278)

Ni muhimu sana kuzingatia suala la adabu na heshima pindi tunapolitembelea kaburi la Mtukufu Mtume (s.a.w), adabu ndio kitu cha kwanza kabisa kinachomfanya muumini kufaidika na hali ya kiroho ya maeneo hayo matukufu.

Siku moja wakati Imam Malik (a.r) alikuwa kwenye mimbari, Abu Jafar Mansur, khalifa wa wakati huo, aliingia msikitini. Alimuuliza maswali Imam na mazungumzo ya kisomi baina yao yakaanzia hapo.

Lakini wakati Abu Jafar Mansur alipoingia sana kwenye mazungumzo hayo na kuanza kuinua sauti yake, Imam Malik alimuonya akimwambia:

"Ewe khalifa! Ishushe sauti yako, kwa sababu Mwenyezi Mungu aliwaonya hata waliokuwa wema zaidi yako. "

Khalifa aliuliza:

"Ewe Imam! Ninapoomba nielekee kwenye Ka'bah au kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w)?" Imam akajibu:

"Kwa nini uweke uso wako mbali naye? Yeye ndiye wasiilah wako na baba yenu Adam (a.s) kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu mpaka siku ya mwisho. Kinyume chake inatakiwa umuelekee Mtume (s.a.w) na kumuombea ili Mwenyezi Mungu Mtukufu amfanye kuwa muombezi wako."[8]

Baadhi ya watu hujifanya vipofu wa kutoliona jambo hili na hawawaruhusu mahujaji kuelekea upande wa kaburi la Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w). Wanasema "mtolee salamu Mtume (s.a.w) na uelekee upande wa Ka'bah;" ilhali Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) yu hai. Kama ambavyo wale waliokufa kishahidi wakiutetea Uislamu wanaendelea kuwa hai, hali ni hiyo

8. Tazama: Qadi Iyad, Shifa-i Sharif, Beirut, 1404, juz. II, uk. 596

hiyo kwa mitume na hususani Mtume Muhammad (s.a.w) ambaye ana daraja kubwa kuliko mashahidi, wanaendelea kuwa hai japo kuwa miili yao imekufa.

Abida al-Salmani alikuwa ni miongo mwa wanazuoni na wasomi wakubwa wa kizazi cha baada ya maswahaba. Alisilimu miaka miwili kabla ya kifo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w). Lakini hakupata heshima ya kukutana naye. Maneno yafuatayo kutoka kwa Abida yanathibitisha upendo wa waumini wa mwanzo kwa Mtukufu Mtume (s.a.w):

"Kupata nywele moja tu ya Mtume (s.a.w) kwangu mie ni fahari kubwa kuliko kuwa na hazina zote za dunia hii." (Ahmad, III, 256)

Mwanazuoni maarufu wa Kiislamu Dhahabi alipoyasikia maneno ya Abida kuhusu upendo wake kwa Mtume (s.a.w), alielezea hisia zake kama ifuatavyo:

"Maneno ya Abida yanaelezea thamani ya nywele moja ya Mtume kuwa kubwa kuliko dhahabu na fedha za ulimwengu huu, ni uthibitisho mkubwa wa upendo aliokuwa nao kwa Mtume (s.a.w). Kama mwanazuoni huyu anasema hayo miaka hamsini tu baada ya kifo cha Mtume, je sisi tutasema nini baada ya miaka mia saba baada ya kifo chake, kama tumepata japo unywele wake,

au kamba ya kiatu chake, au chombo alichotumia kunywea maji?

Je ungemwona tajiri kama mfujaji mali kama atatumia mali yake kupata chombo kama hicho?

Hapana, hapana! Usisite kutumia mali zako zote ili kwenda kuutembelea msikiti wake wenye baraka tele, alioujenga kwa mikono yake mwenyewe, na kupata fursa ya kumtolea salamu nyumbani kwake.

Ukifika Madina, utazame kwa upendo mlima Uhud; kwa sababu Mtukufu Mtume (s.a.w) aliupenda sana. Mara kwa mara tembelea msikiti wake na mahali alipopenda kukaa na jaribu kuulisha moyo wako kwa hali ya kiroho inayopatikana hapo, kwa sababu hauwezi kuwa muumini kamili bila kumpenda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) zaidi ya unavyojipenda mwenyewe, watoto wako, mali zako, na kuliko unavyowapenda watu wote wa ulimwengu…" (Dhahabi, Siyar A'lam al-Nubala, IV, 42-43)

Zama za dola ya Uthmaniya, ambazo ni zama muhimu sana katika historia ya Uislamu baada ya zama za maswahaba na warithi wao, zilishuhudia jamii iliyojaa upendo mkubwa kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w). Hili lilikuwa dhahiri kwa kila raia wa jamii ya Kiuthmaniya kuanzia kwa Sultani hadi kwa wachunga kondoo.

Kwa mfano, kama ilivyo siku hizi, kila linapotajwa jina la Mtukufu Mtume (s.a.w), waumini walikuwa wakimtakia rehma na kuweka mikono yao vifuani mwao kama ishara ya heshima kwake. Washairi waliandika mashairi waliyoyaita mawlid kuyasifu maisha ya Mtukufu Mtume (s.a.w).

Inaposomwa sehemu ya mashairi haya kuhusu kuzaliwa kwake, watu walikuwa wakisimama kuonyesha heshima zao kwa Mtume. Hii ilikuwa kama desturi miongoni mwa Wauthmaniya kuonyesha upendo wao kwa Mtukufu Mtume (s.a.w). Masultan wote wa Kithmaniya wanapoletewa barua kutoka Madina walikuwa wakitawadha kwanza, wakaibusu barua hiyo na kuifuta machoni mwao. Baada ya kufanya hivyo ndipo huisoma barua hiyo huku wakiwa wamesimama.

Wakati wa marekebisho ya msikiti wa Mtume huko Madina, wafanyakazi wa Kiuthmaniya walikuwa makini sana kuhakikisha wanakuwa na wudhu na kusoma *bismillah* (kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehma Mwenye kurehemu) kila wanapoweka jiwe au tofali kwenye jengo hilo. Walikuwa wakifunga vipande vya nguo kuzungu-ka nyundo zao wasimsumbue Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Hizi na nyinginezo ni mojawapo ya adabu za Kiislamu walizokuwa wakizionesha na kuzidhihirisha.

Katika kipindi hiki, Wauthmaniya walikuwa wakituma msafara uliojulikana kama "*sürre alayı*"[9] kwenye mijihii mitukufu. Msafara huo unapofika Madina, ulikuwa hauingii mjini. Walikuwa wakiweka kambi sehemu iliyo karibu na mji kwa usiku mmoja na kujiandaa kimaanawi na kiroho kwa ajili ya kuingia katika mji huo. Baada ya maandalizi hayo ndipo wanapoingia na kufanya ibada zao. Wanaporejea nyumbani walikuwa wakichukua udongo wa Madina na kwenda nao kama sehemu ya *tabarruk*.

Tukizichunguza kwa makini picha za masultani wa Kiuthmaniya, tunaweza kuona kipande cha nyoya juu ya kofia zao. Kuna mtu yeyote aliyekuwa anajua kwamba manyoya haya yalikuwa yanawakilisha ufagio? kwa njia hii masultani wa Kiuthmaniya walikuwa wanaelezea kuwa wao ni watumishi wa ardhi hizo tukufu. Pia walikuwa wakiwalipa mshahara vibarua ambao hufagia sehemu hizi tukufu katika pesa yao wenyewe.

Kuziweka kwa muda mrefu nywele za Mtume (s.a.w) na ndevu zake katika baadhi ya misikiti na

9. Sürre alayı: ni pesa, dhahabu na zawadi mbalimbali ziliokuwa zikitumwa na msafara maalumu kutoka kwa Masultani wa Kiuthmaniya ili zigawiwe kwa watu wa Makka na Madina katika mwezi wa Rajab (Tazama: Münir Atalar, Sürre-i Hümayun ve Sürre Alayları, Diyanet işleri Başkanlığı yayınları, Ankara, 1991,uk. 2)

kuzifunga katika kitambaa kizuri imekuwa ishara ya upendo wa waumini kwa Mtume.

Heshima waliyoionesha Wauthmaniya kwa ajili ya maeneo hayo matakatifu ilikuwa ikianzia ndani ya mji mkuu wa utawala huo. Kwa mfano, watu wa Istanbul wanapokwenda hijjah kutokea upande wa Ulaya wa mji huo, sehemu ya kwanza wanayopita katikaupande wa Asia walipaita *Haram* (eneo takatifu). Kwa njia hii walikuwa wakiandaa mazingira ya kiroho ya kuingia katika *Haramain al-Sharifain* (miji miwili mitakatifu ya Makkah na Madina) mwanzoni kabisa mwa safari yao. Kisha walikuwa hawaruhusu utovu wowote wa adabu au mghafala katika safari yao yote.

Katika muktadha huu, tukio la mwaka 1678 la safari ya hijja iliyofanywa na mshairi wa Kiuthamaniya Naabi akiwa pamoja na wafanyakazi wa serikali ya Kiuthmaniya, ni tukio muhimu sana na la mfano:

Katika safari yake Naabi alimwona afisa mmoja wa Kiuthmaniya akiwa amelala chini na kunyoosha mguu wake kuelekea Madina. Naabi aliumizwa sana na tukio hilo kiasi kwamba alianza kuandika shairi lake maarufu la kumsifu Mtukufu Mtume (s.a.w).

Msafara ulipokaribia Madina karibu na muda wa swala ya alfajiri, Naabi alilisikia shairi lake liki-

somwa kutoka katika minara ya msikiti wa Mtume mjini Madina:

Sakın terk-i edebden kûy-i mahbûb-i Hudâ'dır bu; Nazargâh-ı ilâhîdir, makâm-ı Mustafâ'dır bu!..

"Chunga adabu zako katika eneo hili ambalo hutazamwa na Mwenyezi Mungu na mji wa kipenzi cha Mwenyezi Mungu, Mtume Mustafa."

Murâât-ı edeb şartıyla gir Nâbî bu dergâha, Metâf-ı kudsiyândır, bûsegâh-ı enbiyâdır bu!..

"Ee Naabi! Ingia mahali hapa kwa kuchunga adabu zako. Hili ni eneo lenye Baraka ambalo malaika hulizunguka na huzibusu nguzo za milango yake."

Naabi aliyeshangazwa na kilichotokea, kwa haraka sana akamwendea Muadhini:

"Ni vipi na ni kwa nani umejifunza shairi hili?" Muadhini:

"Usiku wa leo nimemwona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ndotoni. Akaniambia:

"Mshairi aitwaye Naabi kutoka katika ummah wangu atakuja kunitembelea. mshahiri huyu ananipenda sana, kwa sababu ya upendo wake, someni shairi lake katika minara ya msikiti wangu." Kwa hiyo nimetekeleza agizo la Mtume (s.a.w)."

Naabi akaanza kusema kwa kigugumizi:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) amenichukulia kama mmoja katika ummah wake. Jua la ulimwengu wa watu na majini limenikubali katika ummah wake…"

Kwa hiyo jambo la muhimu wakati wa hijjah ni kuwa na hisia adhimu kama hizo wakati wa kumtembelea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kuizunguka Ka'bah.

Kama ilivyo kwa matendo mengine ya ibada, kuitekeleza hijjah katika namna itakayokubaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kunategemea ukamilifu wa imani na utambuzi wa kiroho. Tukiweza kuifanya hijjah yetu kuwa hijjah yenye kukubalika itakuwa ni njia ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu na kutakaswa dhambi zetu. Kwa maneno mengine, matokeo tarajiwa ya ibada hufikiwa tu kwa kuyatekeleza kwa kiwango cha juu kabisa chenye kumridhisha Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Katika hili, maneno yafuatayo ya Shibli (q.s) kwa bwana mmoja aliekwenda kuhijji ni yenye kutuvuta kuangalia kipengele cha kiroho katika hijja na ni ushauri wenye thamani sana na pia ni onyo kwa wale wanaokwenda kuhijji:

"*Unapokusudia kwenda kuhiji, kama haukutubu dhambi zako zote na kurejea katika njia iliyonyooka, basi utakuwa huna nia ya kwenda kuhijji.*

Unapovua nguo zako za kawaida na kuvaa ihram, kama usipovua vyote visivyo na umuhimu, utakuwa bado hujavua nguo.

Unapochukua udhu, kama hukusafisha uchafu wa kiroho na maradhi yote ndani ya moyo, utakuwa hujachukua udhu.

Unapoingia katika msikiti wa Makkah, kama hukuahidi kuacha mambo yote ya haramu yanayokutenganisha na Mwenyezi Mungu, utakuwa hujaingia msikitini.

Unapochinja, kama hukuyachinja matamanio na tamaa zako kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, basi utakuwa hujatoa dhabihu.

Unapompiga mawe shetani, kama hukuupiga mawe ujinga na wasiwasi uliojificha ndani yako na kama hukupata utambuzi ndani ya moyo wako, basi tambua kuwa utakuwa hujampiga mawe shetani.

Ulipofanya safari hiyo, je Baraka za Mwenyezi Mungu zimeongezeka ndani mwako na je, moyo wako umejazwa amani na furaha? Kwa sababu katika maneno ya Mtume imeelezwa kuwa:

"Mahujaji ni wageni wa Mwenyezi MUungu Mtukufu. Ni lazima kwa mwenyeji kuwakirimu wageni wake." Kama hujazitambua dhabihu hizi, ni dhahiri kuwa utakuwa hujaenda kutembelea sehemu hizi tukufu…"[10]

10 Tazama: Ibn Arabī, Al-Futuhat al-Makkiyyah, mhariri ni

Alichojaribu kukielezea Shibli (q.s) ni jukumu la kufuata agizo la Mwenyezi Mungu:

"Timizeni Hija na Umra kwa ajili ya Mwenyezi Mungu…." (Al-Baqara 2: 196)

Jamala za ardhi hizi tukufu na maadili ya waumini wema ambao wanaoishi kwa mujibu wa jamala hizo ndizo zawadi zenye thamani zaidi ambazo mahujjaji wanaweza kurudi nazo nyumbani.

Siku moja kiongozi mmoja wa kidini nchini Pakistani Muhammad Iqbal aliwatembelea mahujaji waliokuwa wamerudi kutoka Madina na kuwauliza maswali yafuatayo:

"Mmeutembelea mji wa Madina. Je mmejaza nyoyo zenu kwa zawadi gani za kiroho kutoka katika soko la Madina? Muda mchache tu kofia, tasbihi, namiswala mliyoileta vitachakaa na kutoweka. Je mme kuja na zawadi yoyote ya kiroho kutoka Madina ambayo haiwezi kuchakaa na kutoweka?

Je unyenyekevu na uaminifu wa Abu Bakr (r.a), udilifu wa Umar (r.a), staha na ukarimu wa Uthman (r.a), na maarifa na ushujaa wa Ali (r.a) ni miongoni mwa zawadi mlizokuja nazo? Mtaweza kuupa furaha na saadah ulimwengu wa Kiislamu unaokabiliwa na matatizo?"

Osman Kahya, Cairo, 1986, X, 133-38

Mwenyezi Mungu Mtukufu atujaalie nuru na utambuzi kamili wa kimaanawi wa kuzitambua ardhi hizi tukufu! Atupatie Baraka ya kufanya ibada ya hijja kwa utambuzi, hisia na ulani wa moyo! Azikubali na azifanye ibada zetu kutokuwa na kasoro, zile ambazo tulizotekeleza na zile tunazotarajia kuzitekeleza. Azifanye kuwa zenye kuendana na misingi hii!

Amin!